# *MUNGU ANAYO NJIA ILIYOWEKWA*

Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa makubwa kuwa hapa usiku wa leo katika ukumbi huu, kuwahudumia watoto wa Mungu, kwa wagonjwa na wanaoteseka, na kuwahudumia wasiookolewa, katika njia ya wokovu. Nasi tunasikitika kwamba huu hauna budi kuwa usiku wetu wa mwisho katika uamsho huu maalum, mfululizo wa ibada hizi, lakini bila shaka tunataka kumshukuru kila mmoja wenu kwa ushirikiano wenu mzuri sana, kwa yote mliyotutendea, kutupa imani yenu, na ninii yenu. . .yote mliyofanya. Tunalithamini kutoka kwenye kilindi cha moyo wetu. Umilele pekee ndio utakaoelezea jinsi tunavyolithamini.

2 Nasi tunataka kumshukuru Ndugu yetu Cauble, kwa kutufadhili hapa mjini; na kwa ushirikiano mzuri ambao tumekuwa nao pamoja naye na kanisa lake, na watu wake. Nasi tunawashukuru ninyi nyote ambao mmetoka sehemu mbalimbali, kutoka Indiana na ujirani, majimbo jirani. Hata haikutangazwa huko nje. Nadhani mlipata tu kwa njia ya barua, kwa namna fulani, ili kuwepo hapa. Maana, tunajua hatungekuwa na nafasi kubwa katika kanisa hilo. Nasi tuliwazia, kama ingekuwa mbaya sana, basi labda tungeweza kupata siku moja au mbili usiku ukumbini.

3 Sasa, tunawashukuru watu walioturuhusu kuutumia ukumbi huu usiku wa leo, tunathamini hilo, kwao kufungua mahali hapa kwa ajili ya ibada hizi Jumapili hii usiku, kwa utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo. Tunamshukuru.

4 Na sasa, nilipokuwa tu nikiingia sasa hivi, ndugu yangu pamoja na Billy, na baadhi yao walikuwa wamesimama pale nje, wakaniambia kuwa kumekuwa na za kutosha, fedha za kutosha kulipia madeni yote. Walilipia kodi ya kanisa, na gazeti, na walinzi wa kanisa, na muziki, na matangazo yote ya magazeti, matangazo ya redio. Kila kitu kimelipiwa, hadi usiku wa leo. Nafikiri walikuwa na za kutosha, kwa hivyo hiyo ikaacha sadaka ya upendo iwe huru kwangu.

5 Hilo, sikuzote nimejaribu kudumisha, kama mjuavyo, sifa kuhusu pesa. Hatufanyi hivyo. Na ikiwa hakuna za kutosha kuyashughulikia mambo, basi nitazitoa kutoka kwenye sadaka yangu ya upendo. Nayo hiyo sadaka ya upendo, hata nisingeichukua, kama sikuwa maskini na ilinibidi kuishi kama wengine wetu wanavyoishi. Kama ningeweza kufanya kazi, na bado niendeshe mikutano hii kote nchini, kamwe nisingetaja

toleo la upendo kwa ajili yangu. Kulipwa kwa matumizi ndiko tu tunakohitaji. Na hiyo haijawa Louisville pekee, hiyo imekuwa ni kote ulimwenguni. Na maadamu niko hai, na Mungu atanisaidia, itabaki hivyo. Si pesa; sifuati pesa. Ninajaribu kuwafanya watu wamwamini Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya wokovu wao na kwa ajili ya uponyaji wao.

6 Nazo zaka zenu, na kadhalika, ambazo mumetoa, juma hili lililopita, zimeenda kwa kusudi hilo. Na Jumapili usiku, wao kwa kawaida, ama usiku wa mwisho wa mkutano, chochote kile, ni juma moja au majuma mawili, siku kumi ama chochote kile, wanachukua sadaka ya upendo kwa ajili yangu. Na kama kungekuwa na kitu mle ndani ambacho kingesalia, kitaenda moja kwa moja kwenye misheni za kigeni. Labda katibu wangu na hao wengine ambao huzitunza hizo pesa, na kadhalika, wapo wameketi sasa, na mke wangu na hao wengine, ambao wanajua ya kwamba hiyo ni kweli. Na Mungu Mwenyezi, aliye Hakimu wetu, anajua kwamba hiyo ni kweli. Na kwa hivyo tunawashukuru kwa kila kitu ambacho mmefanya.

7 Sasa, huu ukiwa ndio usiku wa kumalizia ibada, sasa tutaondoka kesho kuelekea Shreveport, Louisiana, kuanzia kule katika Ukumbi wa Manispaa kwa ajili ya ibada; ibada inayofuata itaanza basi.

8 Na kisha tutoke huko kwenda Denver, Colorado, ambako Wafanyabiashara Wakristo, wa Denver, wanatufadhili huko, katika u—uamsho. Nami ninaamini ni Ukumbi wa Umma ama wa Mji huko; hakuna makanisa yanayoifadhili, ni Wafanyabiashara Wakristo tu.

9 Na kisha kutoka hapo, twende—twende Edmonton, Alberta. Halafu kutoka huko, hadi Grande Prairie, British Columbia; Dawson Creek; tupande kwenda kwenye maeneo ya Eskimo.

10 Kisha tutashuka turudi tena, huku, tuanzie humu majimboni tena, kwenye Juni, ambayo itakuwa huko Des Moines, Iowa. Kisha twende kwenye viwanja vya kambi vya Methodisti kule Cedar Lake, kwenye mkutano kule; na kisha twende kwenye Pasifiki ya Kaskazini Magharibi.

11 Na kisha kutoka huko, hadi Durban, Afrika Kusini. Wakati huu, si chaguo langu, mpangilio wangu. Ni BWANA ASEMA HIVI. Na kwenda Afrika; India; Palestina; Luxembourg; Frankfurt, Ujerumani; na London; na halafu Paris; ndipo turudi nyumbani.

12 Halafu kutoka huko, tunapaswa kuingia mnamo Januari au Februari, twende New Zealand, Australia, na pande za Mashariki.

13 Basi nitakuwa nikitarajia maombi kutoka Louisville, Kentucky, kuunga mkono mkutano huu tunaokwenda, katika ratiba.

14 Moja ya nyakati hizi, kama ikitokea nirudi hata mwaka mmoja kutoka leo, wapo wengi wanaoketi hapa usiku wa leo, labda, hawatakuwa hapa, kama nitaachwa. Katika kusanyiko la namna hii, loo, watu elfu moja au zaidi, wowote wale, kutakuwa—kutakuwako na wengi wenu watakaotoweka. Basi nitakutana nanyi tena, baadhi ya asubuhi hizi tukufu, kwenye ule ufufuo, wakati watakatifu (waliokombolewa) watakaporudishwa duniani tena, kwa ajili ya ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Ninatumaini kukaa nanyi Umilele usio na mwisho katika Ufalme wa Mungu, ambao ninauwakilisha hapa usiku wa leo.

15 Mungu awabariki ninyi nyote. Wala sitaki kumwacha nje mtu yeyote. Maskini hao wasichana wadogo wanaocheza muziki na, loo, kila mtu, Mungu awabariki.

16 Sasa ni kura yangu, usiku wa leo, kuzungumza kwa dakika chache tu tena. Nami sijui ni saa ngapi tunayopaswa kuufunga huu ukumbi. Lakini tunaanza tu kwa wakati, saa mbili u nusu, labda nizungumze nusu saa; kisha tuanzishe mstari wetu wa maombi, tukiwaombea wagonjwa.

17 Na sasa ninyi Wakristo wapendwa hapa, wa Louisville, Kentucky, na Jeffersonville, New Albany. Moja ya siku hizi, ningependa kutangaza mkutano kitaifa, na niwe na maskini hema kubwa limepigwa hapa nje, ambalo litaketi watu elfu kadhaa, na kufanya uamsho wa mtindo wa kale. Huo ndio nafikiri tunahitaji huku Louisville, ni uamsho wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu. Nyinyi ombeni. Bwana akiongoza hivyo, nitakuja.

18 Sasa kuna miamsho miwili ama mitatu ya uponyaji inayoendelea mjini. Ndio maana hatukuwahi kuufanya kuwa jambo la kitaifa. Tumekuja tu kwenye kanisa la Ndugu Cauble, mnaona. Wala hatukuja hapa kuwa washindani wa hawa ndugu wengine. Hatuamini kuwa washindani wa dini ya Yesu Kristo. Sisi ni ndugu, pamoja, tukifanya kazi pamoja kwa yote tuwezayo, kwa manufaa ya Ufalme wa Mungu, na kila kanisa, kila mtu.

19 Tunaweza kutofautiana kidogo juu ya mawazo, wahudumu, lakini sio kwa watu. Tungali tunaamini Damu ya Yesu Kristo hutusafisha na uovu wote. Tunakuwa wana na binti za Mungu kwa kuziungama dhambi zetu na kuikubali Damu hii, haidhuru unashiriki kanisa gani. Nasi tunaamini hilo kwa moyo wetu wote. Ibada zangu daima ni za baina ya kiinjilisti, au zisizo na mipaka ya kimadhehebu, kwa hiyo tunaamini kwamba Mungu atawabariki ninyi nyote.

20 Sasa, katika kusimama, zaidi sana, mjini ama mahali fulani, hatuko hapa kuuwakilisha uponyaji wa Kiungu. Hata hatuupi uponyaji wa Kiungu kipaumbele. Tunampa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kipaumbele. Na unapompa Yesu Kristo kipaumbele,

unaupa uponyaji wa Kiungu kipaumbele. Kwa sababu, ni sifa za mauti Yake, ambayo hutupa wokovu, na uponyaji kwa miili yetu.

21 Wala hakuna—hakuna nguvu ndani ya mtu yeyote, zinazoweza kumponya mtu mwingine. Uponyaji tayari umenunuliwa pale Kalvari. Na jambo pekee tunaloweza kufanya ni kumwelekeza mwanadamu mahali ambapo wakati mmoja, Sadaka itoshelezayo kwa yote ilitolewa na Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Humo ndani, tunatazama tu na kuishi. Mungu alifanya njia, nasi tunaikubali.

22 Mhudumu asingeweza kumwokoa mtu yeyote; angeweza tu kuihubiri Injili, kama ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu, na kuwaelekeza watu mahali walipookolewa. Waliokolewa, miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, pale Kalvari. Inabidi kumkubali kama Mwokozi wako binafsi sasa, upate kufaidika, au kupata mgawo wa faida, kutokana na kifo Chake, na kufurahia sifa za yale aliyoyafia.

23 Sasa, na uponyaji wa Kiungu ni jambo lile lile. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu juu yake, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona," yote katika siku moja, na Mtu yule yule. Isiyotenganika, inaenda sambamba, moja kwa nyingine; Damu inayotoka mgongoni Mwake, na ile inayotoka kwenye jeraha Lake, imechanganyikana na kutiririkia miguuni Mwake. Mnaona, ndivyo hivyo. Wokovu, uponyaji, amani, utoshelevu, furaha, kila kitu tunachohitaji katika safari ya duniani, kililipiwa pale Kalvari. Na Mungu atamhudumia kila mtu ambaye ataikubali juu ya misingi hiyo na kuiamini kwa moyo wao wote.

24 Sasa, "Mungu aliweka Kanisani, wengine waalimu, mitume, manabii, karama za uponyaji," na, loo, aina mbalimbali za karama. Aliliweka hilo Kanisani "kwa ukamilifu wa Kanisa," kulileta Kanisa pamoja.

25 Na sasa, siku zimepita tangu kipindi cha kwanza cha mitume. Walikuwa na karama zote tisa zikifanya kazi kanisani.

Kipindi cha pili, wakaanza kupoa.

Kipindi cha tatu, wote karibu walikuwa wamekwisha.

Ndipo wakaingia kwenye ile miaka elfu moja na mia tano ya nyakati za giza.

Kisha yakaja yale matengenezo.

26 Baada ya hayo matengenezo, ukaja utakaso; baada ya kuhesabiwa haki akaja John Wesley, akihubiri utakaso. Mle ndani akaja Calvini, Knox, na hao wote walioshuka wakaingia kwenye Upentekoste, Nazarayo, wakati huo.

27 Na sasa tunapiga hatua moja kwa moja kuingia katika wakati mwingine mkuu, kuja kwa Kunyakuliwa kwa Kanisa. Na katika huu, tunaishi katika wakati wa kule kurejeshwa kwa karama. Iliyakwaza mengi ya makanisa yao mazuri makubwa;

ilimrudisha Mnazarayo nyuma; ikawafanya Wapentekose wengi sana kuwa walokole. Lakini, vile vile tu, Mungu anaendelea moja kwa moja, akileta Imani ya Kunyakuliwa kwa Kanisa Lake. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, usiku wa leo, ninaiwakilisha Imani hiyo, "Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja," kwa njia ya karama ya Kiungu.

28 Ambayo, nionavyo mimi, "Karama na miito . . . " Sio maoni yangu; lakini Biblia inasema, kwamba, "Karama na miito havina majuto." Hakuna kitu unachoweza kufanya kulihusu. Huwezi kujipa macho ya bluu wakati ukiwa na ya kahawia. Wewe uko tu jinsi ulivyo, kwa neema ya Mungu.

29 Huwezi hata kumjia Mungu bila Mungu kukuita kwanza. Huwezi kumtafuta Mungu pasipo Mungu kukutafuta wewe kwanza na kukuita. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu." Kwa hiyo, Mungu anatafuta. "Mungu ameweka Kanisani . . . "

30 Na basi kutoka kwa mtoto mdogo, aliyezaliwa hapa katika jimbo hili la Kentucky, maono hunijia tu kama vile tu—kama vile kula au chochote kile. Ni vile tu Mungu apendavyo, Yeye anayatoa. Ninafanya tu vile Yeye anavyoniambia nifanye.

31 Bila shaka, nina wakosoaji wengi. Nina watu wengi wasioyaamini. Haidhuru ni nini kingetukia, wasingeamini, kwa vyovyote vile. Natarajia kuwa na hao. Na kama sikuwa nao, ningeshuka madhabahuni mahali fulani na kusema, "Bwana mpendwa, nina shida gani?"

32 "Na wote wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu watateswa." Kweli. Lazima tuyapate. Hiyo ni kweli.

33 Kwa hiyo, Yesu aliyapata. Naye akasema, kama . . . Wakati angeweza kusimama katika kusanyiko Lake, na kujua shida za (watu) na endapo walipona au hawakupona. Nao wakamgusa, kwa imani ya—yao. Alipogeuka na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Alisema, "Imani yako imekuokoa. Sasa kutokwa kwako damu kumekoma. Imani yako imekuponya."

34 Mwanamke alimjia wakati mmoja. Ama, Yeye alikuwa amesimama pale alipokuwa; kwenye kidimbwi, ama mahali pa kunywea, kisima, kisima cha Yakobo. Ndipo mwanamke akaja, naye akafanya mazungumzo naye kwa dakika chache mpaka akagundua shida yake. Kasema, "Nenda kamwite mumeo."

Akasema, "Sina yeyote."

Kasema, "Hiyo ni kweli. Unao watano."

35 Yeye, Yeye alipokuwa hapa, alijua mahali samaki alipokuwa, aliyekuwa na sarafu kinywani mwake. Alijua mahali ambapo nyumbu wawili walikuwa wamesimama, wamefungiwa, kwenye makutano ya njia mbili. Naye alijua mahali ambapo mtu angekuwa amebeba mtungi. Mambo mengi ambayo Yeye alijua. Alimjua Filipo alipomjia, ya kwamba alikuwa akiomba kabla

hajaja, chini ya mti; alijua kwamba alikuwa mtu mwema, mwenye haki.

36 Lakini Yeye alisema, kwa Maneno Yake Mwenyewe, "Siwezi kutenda lolote kwa nafsi Yangu, mpaka Baba anionyeshe la kufanya." Wote wanaoamini Maandiko hayo, semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hivyo ndivyo, Yohana Mtakatifu 5:19.

37 Alipita karibu na umati mkubwa, watu elfu mbili ama tatu mle ndani; viwete, waliopinda, wasiojiweza, vilema, vipofu, waliopooza; amejaa upendo na huruma, akampita kila mmoja wao. Akamponya mtu mwenye ugonjwa fulani ulioonekana mdogo. Loo, sijui; inawezekana alikuwa mwepesi wa kushikwa na homa mbaya, nijuavyo mimi. Huo, alikuwa nao kwa muda wa miaka thelathini na minane. Haungemdhuru wala kumwua; ulikuwa umedumaa. Naye akamponya mtu huyo, kisha akaenda zake na kuuacha umati huo umekaa hapo. Ndipo alipoulizwa, alisema, "Siwezi kufanya lolote kwa nafsi Yangu, ila lile nimwonalo Baba analitenda."

38 Sasa wakati mwingine watu wanataka kufanyia hilo mzaha, walipoona Yeye alikuwa na nguvu hizo. Wakamwuliza. Herode akasema, "Nifanyie mwujiza. Hebu nione ukifanya kitu." Kisha akamwomba ajitetee. Akasimama, kama, kimya mbele ya wamkatao manyoya, kama kondoo alivyo kimya mbele ya wamkatao manyoya.

39 Walimfunga kitambaa kichwani Mwake, siku moja, kundi la askari wakosoaji, wakampiga kichwani, na kusema, "Sasa kama Wewe ni nabii, kama unajua mambo haya yote, na kadhalika, tuambie ni nani aliyekupiga. Tufanyie mwujiza."

40 Shetani alipokutana Naye mara ya kwanza, Shetani alisema, "Sasa kama utanifanyia mwujiza, nitaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Geuza mawe haya yawe mkate. Hebu nione ukifanya hivyo."

Yesu alimnukulia tu Maandiko moja kwa moja tena.

41 Na halafu, kila wakati, Shetani alitaka kumwona akifanya mwujiza. Watu waliopagawa na Shetani, wanataka kumwona, "Nifanyie kitu. Hebu nikuone Wewe ukimponya *huyu*. Acha niukwaruze mkono Wako; kisha uuponye nami nitakuamini." Haya basi. Pepo mchafu yuyo huyo aliyesema, "Shuka msalabani sasa nasi tutakuamini. Mikono Yako imepigiliwa hapo juu. Unamwita Eliya; hebu tumwone akija, akukomboe sasa. Ikiwa umepata kibali sana Kwake, kwa Mungu, hebu tumwone Yeye akikukomboa. Shuka msalabani nasi tutakuamini. Fanya mwujiza mbele yetu."

42 Miujiza daima imewakwaza wasioamini. Lakini, vivyo hivyo, Baba yetu wa Mbinguni ni Mungu atendaye miujiza, hata hivyo. Ndivyo hivyo. Kila mahali Yeye amekuwa daima, vyovyote

huduma Yake imekuwa, mahali ambapo amekuwa na wahudumu Wake, kumekuwa na ishara, maajabu, na miujiza.

43 Sasa Bwana awabariki, ninaposoma somo la Maandiko hapa kwa dakika chache, na ndipo tutaingia kwenye ibada, na kisha moja kwa moja kwenye ibada ya uponyaji.

44 Sasa tazama. Yesu, alipokuwa hapa duniani, alisema, "Sasa, mambo niyafanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya. Zaidi ya haya mtafanya, ama makubwa zaidi, kwa maana Mimi naenda kwa Baba Yangu. Sasa bado kitambo kidogo," ninamnukuu Yesu, "bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

45 Ni Wakristo wangapi humu ndani, usiku wa leo, wanaoamini kwa moyo wenu wote, kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu na yu hai usiku wa leo? Hebu tuone mkono wako. Vema, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, si atazalisha, usiku wa leo, katika Kanisa Lake, jambo lile lile alilofanya Kanisani Mwake, alipokuwa hapa duniani, katika mwili? Mnaona? Ni ninii tu . . . Roho Mtakatifu ni Roho wa Yesu Kristo. Yuko hapa katika umbo la kiroho, akiwa hai tu kama alivyowahi kuwa; hapa, akiishi ndani yetu, akifanya mambo aliyofanya alipokuwa hapa duniani, kama thibitisho la Yeye kuwa pamoja nasi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu." Bwana awabariki.

Na tuombe.

46 Baba wa Mbinguni, usiku wa leo, pata utukufu, Baba wa Mbinguni, kutokana na juhudi zetu tunazojaribu kutoa kwa ajili ya utukufu Wako. Sasa hili hapa Neno limewekwa, hapa mimbarani, limefunguliwa. Lakini ni nani anayeweza kulielewa? Wakati, limeandikwa kwa uvuvio, limeahidiwa, kwamba, "Lilifichwa kutoka kwa macho ya wenye hekima na busara, nalo lingefunuliwa watoto wachanga ambao wangeweza kujifunza." Sasa, Baba, tunaomba ya kwamba utatujalia tujihesabu kuwa watoto wachanga, wasiojua lolote, tupate kujifunza mambo fulani kupitia kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu. Jalia alichukue Neno la Mungu sasa na alipe kila moyo sawasawa na mahitaji yetu. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

Katika Mwanzo . . .

47 Joto kidogo tu hapa; nadhani ni vivyo hivyo hapo nje, pia. Ikiwa wasimamizi watafungulia hewa kidogo ndani ya jengo, ili watu wajisikie vizuri kidogo. Naona baadhi yao wakipepeta.

48 Sasa, katika Mwanzo mlango wa 22, ninataka kuuvutia usikivu wenu kwenye maneno machache hapa; mwishoni tu mwa mkutano huu, wa Injili. Daima napenda kusema, ama kusoma

baadhi ya Neno hapa, kwa maana Neno hili halitapita kamwe. Na ni la Milele, daima.

49 Na kama ningesema lolote kuhusu somo, la usiku wa leo, ningetaka kuzungumza juu ya hili: *Mungu Anayo Njia Iliyowekwa*. Anayo njia iliyowekwa ya kumkaribia. Anayo njia iliyowekwa ya kuepukia. Pia anayo njia iliyowekwa kwa kila kitu tunachohitaji. Laiti tungeweza kupata njia hiyo ambayo Mungu ameiweka, ndipo tuna hakika ya kuipata. Iwapo Mungu. . .

50 Kama jengo hili lilitolewa hapa ili kushughulikia, kutukinga na mvua; maadamu tunaingia humu jengoni, basi tumetoka kwenye mvua.

51 Ikiwa Mungu ameweka njia ya wokovu, tukiweza kuipata njia hiyo iliyowekwa, tunaweza kupata wokovu. Kama Mungu ameweka njia ya uponyaji wa Kiungu, basi tunaweza kupata, kuingia katika njia hiyo, tunapata uponyaji wa Kiungu. Kama ametoa amani kwa wasio imara, basi kama tukiingia katika njia hiyo na kutafuta njia Yake iliyowekwa, tunaweza kuwa na amani.

52 Sasa tukisoma kutoka kifungu cha 7 cha mlango wa 22. Angalieni hii sasa; hadithi kuu ya kusisimua hapa mbele yetu.

> *Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akanena,. . . baba: akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama, moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?*
>
> *Ibrahimu akasema, Mwanangu, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa:. . .*

53 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno hilo. Huenda nikasoma, katika kujibia hilo, aya ya 14, pia.

> *Ibrahimu akapaita mahali hapo Yohova-yire: kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa Bwana itaonekana.*

54 *Yehova-yire* lilikuwa ndilo jina la Mungu la ukombozi. Mungu, neno *Yehova-yire,* maana yake, "Mungu atajipatia Mwenyewe dhabihu." "Mungu atafanya njia," vinginevyo. Sasa, Mungu alikuwa na majina saba ambatani ya ukombozi; Yehova-yire, na Yehova-manase, na Yehova-rafa, Mponyaji, na majina haya yote ambatani mbalimbali aliyokuwa nayo, kile alichokuwa, yakiwakilisha kile alichokuwa kwa watu. Na hii dhabihu iliyotolewa, usiku wa leo, *Yehova-yire,* "Bwana atajipatia Mwenyewe mwana-kondoo."

55 Ile hadithi kuu ya kuchangamsha iliyowekwa mbele zetu, tu—tunapoingia sasa, Roho Mtakatifu na ayachukue Maneno haya machache yanayofuata na kufunga kila moyo.

56 Sasa huu ndio usiku wa mwisho wa ibada, nami nataka kila mmoja wenu anipe usikivu wenu mkamilifu, na msikilize kwa

makini sasa. Tunajaribu kuingia kwenye ushindi ulio mkubwa zaidi wa huu mkutano. Huu ndio usiku wa mwisho. Kwa kawaida kuna watu wengi zaidi wanaoponywa kwenye usiku wa mwisho kuliko kwenye mkutano wote; matarajio makubwa.

57 Shetani anapiga vita zaidi. Kila kitu kinakwenda vibaya, inavyoonekana, kwa sababu Shetani anajaribu kuwatia watu hao wasiwasi, na kila kitu, ili aweze kuwaepusha na wakati huu mkuu wa msukumo tunaoingia sasa, kwa ajili ya ninii kuu, kama tunavyoweza kusema, "Kuuendea ule ushindi mkuu sasa."

58 Tayari amesukumiwa, pembeni. Amefichuliwa, na hila zake zote zimefichuliwa. Na wanaume kwa wanawake wamemkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wao. Watu wanaougua kansa na vivimbe, na—na kila kitu kingine, wameponywa; taarifa za madaktari zikithibitisha kwamba ni kweli.

59 Sasa hili hapa kundi la watu limeketi hapa usiku wa leo, wameketi, wakingojea chini ya matarajio makubwa sana. Naye Shetani, kama anaweza kukatiza nia yako, hilo ndilo tu limpasalo kufanya. Lakini hebu tuingie ndani sasa tupate ushindi mkubwa, sasa hivi, kumfukuza Shetani na nguvu zake zote moja kwa moja kutoka kwenye hili jengo, kusudi Mungu aweze kupata njia sahihi na kuponya kila mgonjwa, kwa utukufu wa Mungu.

60 Sasa, mzee Ibrahimu alishuka kutoka Shinari, mbali na mnara wa Babeli. Yeye na baba yake walisafiri wakashuka kwenye nchi—nchi tambarare. Na hapo, Ibrahimu, akiwa na umri wa yapata miaka sabini na mitano, Mungu alimwita Ibrahimu, kwa uteuzi, na kumtuma nje ya nchi yake, akimwambia kwamba atapata mtoto kwa mkewe, Sara, ambaye alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano wakati huo. Mungu aliahidi. Nawataka muone jinsi ahadi za Mungu zilivyo halisi kwa wale watakaozikubali. Naye akamwambia atakalofanya. Naye akaondoka, asijue aendako, lakini akakaa katika nchi ya ugenini.

61 Mungu, anapowaita watu, huagiza utengano mkamilifu kutoka kwa mambo yote ya ulimwengu; kuangamizwa kwa mambo ya kidunia. Jitenge mwenyewe, na Mungu atakubariki. "Tokeni kati yao; msishiriki dhambi zao." "Msijifunge nira kati ya wasioamini, bali jifungeni nira pamoja na waaminio, raia wenza wa Ufalme."

62 Naye Ibrahimu ilimbidi kumchukua mkewe na kuondoka humo nchini. Lakini alimwamini Mungu, kwa imani. Usingeweza kulihoji. Hakuna njia ya kupata jinsi angeweza kulifanya. Jinsi, mwanamke huyu, alivyoishi pamoja naye tangu alipokuwa msichana mdogo; wote wawili, vijana, watu wenye afya njema, siku hizi zote; mpaka alipokuwa na umri wa miaka arobaini, hamsini, sitini, pengine miaka ishirini na mitano baada ya kukoma hedhi. Naye Mungu akasema, "Utapata mtoto

kwa mwanamke huyu." Naye Ibrahimu akamwamini Mungu; dhidi ya hoja zote, dhidi ya utafiti wote wa kisayansi, hata wa leo. Mwanamke angewezaje, mwenye umri wa miaka sitini na mitano, kuzaa mtoto? Lakini Mungu alisema angemzaa, kwa hiyo Ibrahimu akaamini hilo.

63 Basi akatoka, bila kujua alikokuwa anaenda. Na, hatimaye, baada ya Sara kupata umri wa karibu miaka mia moja, Ibrahimu angali akiamini. Nawatakeni mlione. Akiwa bado anaamini kwamba Mungu alikuwa anaenda kutimiza ahadi Yake, alikuwa ameandaa kila kitu kwa ajili ya mtoto huyo. Basi hatimaye huyo kijana akawasili. Mungu daima hulifanya hivyo. Alimleta huyo mtoto kwa wakati ufaao.

64 Mnaona, kadiri ilivyochukua muda mrefu, ndivyo Ibrahimu alivyowazia, "Naam, sikumpata leo. Sikumpata mwezi huu. Sikumpata mwezi uliopita. Lakini haidhuru itachukua muda gani, jinsi inavyochukua muda mrefu, kadiri ninavyozeeka, ndivyo itakavyokuwa ni mwujiza mkubwa zaidi." Mpeni Mungu sifa kwa ajili yake.

65 Badala ya kuwa dhaifu, kama vile tungekuwa; kuombewa, usiku wa leo, na ku—kupona; kasema uliugua zaidi kesho yake, unasema, "Loo, vema, hakuna kitu kwake." Hiyo ndiyo sababu; huwezi kulishika Neno la Mungu.

66 "Neno Lako nimelificha moyoni mwangu, Ee Bwana!" Daudi! Ficha Neno la Mungu moyoni mwako, na ndipo Mungu atalitimiza Neno hilo. Mungu hana budi kulitimiza Neno Lake. Haimbidi Mungu kuponya, kuthibitisha nguvu Zake. Bali hana budi kuponya, kulitimiza Neno Lake. Hiyo ni kweli. Haimbidi Mungu kuthibitisha chochote. Yeye ni Mungu. Lakini kile anachonena, Yeye anawajibika kwa Neno Lake. Vivyo hivyo wewe na mimi tunawajibika kwa neno letu. Naye Mungu anawajibika kwa Neno Lake.

67 Kwa hiyo kama uponyaji wa Kiungu uko katika Neno, hilo latosha. Kama "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa," hiyo ilikuwa ni dhabihu, hiyo yatosha. Kwangu mimi, hilo latosha. Kama Mungu alifanya jambo hilo pale, akaahidi angelifanya, hilo latosha.

68 Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Ibrahimu. Lije lisije, Ibrahimu aliliamini kwa vyovyote vile. Labda aliandaa kila kitu kwa ajili ya huyo mtoto, ndipo Mungu akamwacha aendelee mpaka alipokuwa na umri wa miaka mia moja; akambadilisha yeye na Sara kuwa kijana mwanamke, kijana mwanamume tena, na kuwapa huyo mtoto mchanga.

69 Hapo, ni picha nzuri jinsi gani sasa tuliyo nayo mbele zetu, tunayoizingatia. Huyu hapa huyo mtoto, anafikia yapata umri wa miaka kumi na sita, kumi na saba, kipenzi chenyewe cha huyu mwanamume na mwanamke wakongwe; anapendeza, huyo jamaa mdogo.

70 Sasa Mungu anazungumza na Ibrahimu, usiku mmoja, kasema, "Ibrahimu, mchukue umpeleke kule mlimani, kisha umtoe sadaka. Umwue." Na, hata hivyo, Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu, ya kwamba, "Kupitia Isaka mataifa yote ya ulimwengu yangebarikiwa." Atafanyaje sasa, baada ya miaka yote hii wakingojea, akiamini; na sasa baada ya muda wote huu kupita, huyu mtoto. . . Tumaini pekee la ahadi ya Mungu, naye Mungu akamwambia Ibrahimu aharibu kila tumaini alilokuwa nalo tena.

71 Mnaona jinsi Mungu afanyavyo? Majaribio! Mungu wakati mwingine hukuruhusu kuugua zaidi ukiisha kuombewa, apate tu kukujaribu. Majaribio na kujaribiwa kwa imani! Lakini, "yeye atakayevumilia." Hilo hapo. Shikilia; amini Neno la Mungu. Amini kila Neno Lake. Haidhuru kitu kingine chochote kinasema au kinafanya nini; liamini Hilo, kwa vyovyote vile. Haidhuru hali ya mambo inaonekanaje; mwamini Mungu, kwa vyovyote vile.

72 Ndipo, hapo Mungu anasema, "Mchukue huyo mvulana ukampandishe huko juu. Nitaubariki ulimwengu wote kwake. Umengojea kwa miaka hii yote; sasa una umri wa miaka mia moja, yapata umri wa miaka mia moja na kumi na sita, kumi na minane. Sasa nataka umchukue jamaa huyo mdogo, na umpandishe mlimani kule umwue."

73 Jamani, loo, lilionekana lisilo la kawaida kabisa, lisilo na busara, kwamba Mungu angemwagiza Ibrahimu kumwangamiza mwanawe wa pekee. Lakini, nyuma yake sasa, tunaona picha aliyokuwa akichora; Mungu akimtoa Mwanawe wa pekee.

74 Ibrahimu hakutaka kumwambia mama yake, bila shaka, ingemvunja moyo. Akawatandika nyumbu kadhaa, na kuchukua watumishi wachache, kisha akaelekea mlimani.

75 Ninapenda tu sehemu hii hapa. Kisha akapanda mlimani, akamwambia mtumishi, "Ngojeni hapa sasa, wakati mimi na mvulana huyo tukipanda kule tukaabudu. Nami na mvulana tutarudi."

76 Atarudije, wakati alikuwa anaenda kumwua? Lakini Ibrahimu alijua hili, kwamba, "Alikuwa amempokea kama mfano, kama mtu kutoka kwa wafu, naye Mungu alikuwa na uwezo wa kumfufua katika wafu." Mungu angeandaa njia ya kuepukia, kwa namna fulani. Kwa njia gani, yeye hakujua. Mungu alimwambia, mchukue ukamwue, na hilo ndilo jambo pekee alilopaswa kufanya.

77 "Ninyi ngojeni hapa. Mimi na mvulana tutakwenda kule tukaabudu, nami na mvulana tutarudi."

78 Angalia, maskini Isaka aliokota kuni, akapanda mlimani. Baba, akiongoza; Isaka, nyuma, na kuni mgongoni mwake. Iangalie, picha nzuri ya miaka mia nane baadaye, Mungu

akimwongoza Mwanawe Mwenyewe pale juu Kalvari, huku amebeba mbao mgongoni Mwake, kwa ajili ya dhabihu. Picha, Mungu akifanya njia ya kuepukia.

79 Sasa, na wakati Ibrahimu alipopanda juu ya mlima, alifingirisha mawe pamoja na kujenga madhabahu, akaziweka kuni chini; maskini mtoto mdogo alisema, “Baba?”

Akasema, “Mimi hapa, mwanangu.”

80 Akasema, “Madhabahu yapo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo wa sadaka?”

81 Naye Ibrahimu, kwa sauti ya kutetemeka, akasema, “Mungu atamtoa mwana-kondoo kwa hiyo dhabihu.” Angalia wakati huo wenye giza. Walakini, imani, isiyoghoshiwa, isingemwacha asimwamini Mungu. Angalia. Loo, mimi huitazama tu hadithi hii wakati mwingine na kulia kwa furaha.

82 Ibrahimu akaufunga mkono wa mwanawe mwenyewe, akamlaza juu ya madhabahu; akachomoa kisu kutoka kwenye mshipi wake, naye alikuwa tayari kuutoa uhai wa mwanawe, kwa sababu Mungu alikuwa amemwambia afanye hivyo.

83 Ndipo wakati huo, Sauti ilipazwa kutoka Mbinguni, ikasema, “Ibrahimu, usiunyoshe mkono wako!” Ndipo Roho Mtakatifu alipoushika mkono wake, alisema, “Naona hukunizuilia mwanao mwenyewe. Najua unanipenda Mimi.”

84 Na yapata wakati huo, kitu fulani kilianza kulia nyikani, kimenaswa kule, na huyo hapo maskini kondoo dume. Mungu alitoa dhabihu.

85 Tazama, “kondoo dume.” Ilibidi awe kondoo, dume, kondoo dume. Mfano wa Kristo, ambaye angepachukua mahali pa mauti. Hiyo hapo Dhabihu ya Mungu iliyotolewa. Basi Ibrahimu akatoa hiyo dhabihu badala ya Isaka. Ni picha nzuri jinsi gani sasa! Angalieni, Mungu daima alifanya njia. Atafanya njia, usiku wa leo, kwa kila mmoja wenu.

86 Nao Israeli, walipokuwa huko chini Misri, walikuwa katika utumwa na katika taabu, nao wakaanza kumlilia Mungu awakomboe. Angalieni, jinsi Mungu atakavyotoa ni tunapokuwa katika Neno la Mungu. Israeli walikuwa na Neno la Mungu kwamba watatoka huko, siku moja. Kwa hiyo, wakaanza kumlilia Mungu, kulingana na mapenzi ya Mungu, ili Mungu awape kile alichokuwa ameahidi kufanya.

87 Haya basi. Unaombea kitu ambacho kiko nje ya mapenzi ya Mungu, huwezi kuwa na imani kwa ajili yake. Lakini Mungu anapoahidi chochote, ninaamini ya kwamba atatimiza Neno Lake. Kwa hiyo, walijua.

88 Hiyo ndiyo sababu Ibrahimu alijua ya kwamba Mungu atamkomboa, kwa njia fulani, kwa sababu alikuwa ameahidi kwamba kupitia Isaka, mataifa yote ya ulimwengu yatabarikiwa.

89 Wana wa Israeli, kule chini Misri, walijua Mungu alikuwa amewaahidi ukombozi, kwa hiyo wakaanza kuiombea hiyo ahadi.

90 Unasema, "Ndugu Branham, laiti ningalijua uponyaji wa Kiungu, ya kwamba Mungu alikuwa ameuahidi!"

91 Vema, hebu tuuchukue kwa muda kidogo, Yakobo 5:14. Kama hakuna uamsho wa uponyaji mahali fulani mjini, alisema, "Akiwapo mtu yeyote miongoni mwenu, mgonjwa, na awaite wazee wa kanisa; wampake mafuta, na kuwaombea. Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo." Hilo ni Neno la Mungu, njia ya Mungu iliyoandaliwa. Hiyo ni kweli.

92 Angalieni wakati Israeli walipoanza kulia. Mungu alianza kusikia, na kufanya njia ya kuepukia; akawatumia Musa. Ilikuwa ajabu jinsi gani, baada ya kulilia ukombozi; basi walipoletewa ukombozi, walishindwa kuutambua, nao wakaukataa, ndipo ikawabidi kuteseka miaka arobaini zaidi.

93 Je, huo si ni mfano wa siku hizi? Mungu atakuletea kitu fulani, nawe utakiogopa.

94 Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kwenu ninyi watu msiolipenda kanisa hili lote rasmi, dini za matambiko. Mungu alikutumia Roho Mtakatifu; makundi makubwa yao yanamwogopa.

95 Wanafunzi walikuwa karibu kuzama, usiku mmoja, ndani ya chombo kidogo, nacho kikarushwa-rushwa huko baharini, nao wakapiga kelele kuomba usaidizi. Basi walipomwona yule Mtu pekee ambaye angeweza kuyakomesha mawimbi, akija, walimwogopa na kuwazia Yeye alikuwa mzimu. Tumaini pekee walilokuwa nalo; walimwogopa.

96 Kunao wanaume na wanawake wanaoketi hapa usiku wa leo, wenye kansa, ugonjwa wa moyo, magonjwa hatari, hapana shaka. Na tumaini pekee mlilo nalo. . . baada ya daktari wenu kufanya—kufanya yote awezayo kufanya. Mnaogopa tu kumfikia na kumwamini.

97 Usiogope. Chukua Neno Lake. Simama moja kwa moja hapo nje. Ni njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili yako. Mungu alikutuma hapa, usiku wa leo, kwa kusudi hilo. Yeye kamwe hakukutuma hapa, usiku wa leo, ili mimi nikuombee. Alikutuma hapa, usiku wa leo, kuikubali njia Yake iliyowekwa, Yesu Kristo Sadaka ya upatanisho kwa ajili ya dhambi na magonjwa. Natumaini mnalipata.

98 Angalieni, walililia ukombozi. Mungu akawapelekea ukombozi. Ilibidi wangojee miaka arobaini tena kuupokea.

99 Huko nyikani, Mungu aliahidi kwamba angewapa kila kitu walichohitaji. Wakaishiwa na mkate. Naye Yehova-Yire yeye yule, "Mungu atatoa dhabihu," kwa Ibrahimu; miaka mia

nne baadaye, angali alikuwa ni Yehova-Yire, kutoa kila kitu ambacho watoto Wake walikuwa wanahitaji.

100 Hili hapa. Ninataka lizame ndani kabisa upande wa kushoto, chini ya ubavu wa tano. Sikilizeni. Yeye angali ni Yehova-yire, dhabihu ya Bwana iliyotolewa. Ikubali. Usijaribu tu kulihoji. Usijaribu kutoa hoja; huwezi kutoa hoja. Njia za Mungu hazitafutiki. Humhoji Mungu. Humjui kwa maarifa. Humjui kwa elimu. Unamjua kwa kitu kimoja tu, imani. Huwezi kutoa hoja. Sio busara kuamini kuwa unaweza kulihoji. Huwezi. Inabidi tu ulikubali.

101 Angalieni, tena, katika wakati huu mkuu, wa ajabu sana. Waliishiwa na mkate. Watafanya nini? Kama Mungu aliwaambia wangeenda kwenye nchi ya ahadi, ni juu ya Mungu kuwatunza mpaka wafike huko. Na Yehova-Yire Mwenyewe alikuwa papo hapo pamoja nao. Na ndipo walipoishiwa na mkate, Yehova-Yire aliweka njia ya mkate, kote kupitia nyikani. Mana ilinyesha kutoka mbinguni.

102 Wakaishiwa na maji. Kuna faida gani ya kuhofu? Yehova-Yire, dhabihu ya Bwana iliyotolewa, alikuwa papo hapo pamoja nao. Naye akaupiga ule mwamba. Nao wakanena nao, tangu hapo na kuendelea, nayo maji yakatokea kwa wingi. Wakawanywesha ng'ombe wao wote, maelfu ya galoni kwa sekunde, yakibubujika kutoka kwenye mwamba katika jangwa kavu. Halina busara, sivyo? Lakini Mungu aliweka. Huhoji jinsi Yeye hufanya hivyo. Yeye hulifanya tu kwa sababu alisema atalifanya.

103 Inawezekanaje mgonjwa, aliyelala, akifa kwa kansa, madaktari walio bora zaidi wakisema kwamba hakuna tumaini hata kidogo, wangewezaje kupona? Halina busara. Lakini Yeye ni Yehova-Yire, dhabihu ya Bwana iliyotolewa. Ni nzuri jinsi gani!

104 Siku moja, walipata ugonjwa kambini. Hawakuwa na, pengine, hakuna wataalamu wa tiba wala matibabu. Ilikuwa nini . . . Musa huko nje pamoja na kundi hilo lote la watu, milioni mbili hivi, wazee kwa vijana, na wagonjwa na kadhalika; walipotoka nyikani, hapakuwapo na mnyonge miongoni mwao. Lakini sasa angalieni walipokuwa huko nje, nao wakatenda dhambi, nao nyoka wakaanza kuwauma, hakuna lolote wangeweza kufanya. Ndipo Mungu, na wakati Musa alipokuwa akizungumza Naye, alitoa upatanisho; akamwambia Musa, "Nenda kachukue kipande cha shaba. Fanya nyoka kwake, na kuiweka juu ya mlingoti. Na itakuwa, yeyote atakayeitazama nyoka hii atapona."

105 Mfano mzuri, tena. Ile shaba, nyoka yenyewe, ilinena juu ya dhambi iliyokwisha kuhukumiwa; Edeni, wakati Mungu alipotangaza hukumu juu ya yule nyoka, alikuwa tayari ameshahukumiwa.

106 Shaba inazungumza juu ya hukumu ya Kiungu, kwenye madhabahu ya shaba ambapo miili ya wanyama iliteketezwa. Baada ya damu kuchukuliwa; kila saa tatu asubuhi, saa sita na saa tisa alasiri, galoni za damu zilitupwa kwenye madhabahu hii, juu ya miili ya wale wanyama waliokufa, moshi mweusi ukapanda juu. Kila Myahudi kule Palestina akaanguka miguuni mwake, na mikono yake imeelekea Mbinguni; na, moshi huo ulipokuwa ukipaa juu, maombi yake yaliambatana nao. Vema. Hukumu ya Kiungu; miili hiyo iliteketezwa juu ya madhabahu ya shaba.

107 Kama tu katika Israeli, wakati Ahabu alipokuwa amewafanya Israeli kutenda dhambi. Ndipo Eliya akatoka ili kuzitazama anga; miaka mitatu na miezi sita, bila mvua. Akasema, "Inaonekana kama shaba," hukumu ya Kiungu.

108 Katika Ufunuo, walipomwona Yesu, katika Ufunuo 1, "Miguu Yake ilionekana kama shaba," hukumu ya Kiungu.

109 Ile nyoka ilinena juu ya hukumu ya Kiungu, na kumridhisha Mungu. Hukumu Zake ni za Kiungu. Na, tena, hiyo nguzo iliwakilisha msalaba. Nayo nyoka ikamwakilisha Yesu, Bwana Yesu mpendwa; Yeye alishuka na kufanyika dhambi. Mungu Mwenyewe alijifunua katika mwili, uliofanyika kama mwili wenye dhambi, ili kuondoa magonjwa na dhambi ulimwenguni. Ni nzuri jinsi gani! Mle ndani alifanya njia. Yesu alisema, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba nyikani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa."

110 Sasa ile nyoka ya shaba iliinuliwa kwa sababu gani? Kwa sababu maradufu. Walikuwa wametenda dhambi na walikuwa ni wagonjwa. Sasa, basi, Yesu aliinuliwa juu, "akajeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tumepona," sababu maradufu. Na bado ni halisi tu, usiku wa leo, kwa Kristo kuwaponya wagonjwa, kama ilivyo kuwaokoa wenye dhambi.

111 Ni mwujiza zaidi Kwake kumwokoa mwenye dhambi; inambidi Yeye kuzibadilisha njia zake. Na, hakika, akiisha kubadilishwa, angejua jinsi ya kumwamini Mungu kwa ajili ya uponyaji wake. Mnaona ninachomaanisha?

112 Mfano mwingine mzuri, upesi, ilitokea kwamba niliwazia, katika Kitabu cha Ruthu. Wengi wenu mnakipitia Kitabu hicho haraka; hamwazii, pasipo kuwazia ni kitu gani. Hicho ni mojawapo ya hadithi kuu sana mle, za mfano wa Kristo, katika Agano lote la Kale.

113 Katika mlango wa kwanza wa—wa Kitabu cha Ruthu. Naomi, neno *Naomi,* maana yake ni "kupendeza." Yeye, mumewe, na wanawe wawili, waliondoka Palestina, mfano wa kanisa. Nao wakaondoka Palestina, wakahamia nchi ya Moabu. Na huko wakafanya makao, nje ya nchi ya uenyeji wao. Huo ni mfano wa kurudi nyuma, kama Israeli walivyofanya. Myahudi yeyote aliyeondoka Palestina alikuwa nje ya mapenzi ya Bwana.

Mungu aliwapa Wayahudi Palestina, kisha akasema: "Kaeni humo." Naye Ruthu akaondoka . . . au, sio Ruthu, bali Naomi.

114 Nao wanawe wawili wakaoa. Ndipo wanaume wote wakafa; mumewe na wanawe wawili. Akaanza kurudi nyumbani kwake. Wakwe zake wakasafiri naye kidogo. Mmoja wao akainua macho yake na kuangalia nyuma nchini mwake; akarudi. Lakini Ruthu, Mmoabu, asingeweza kwenda. Alimpenda mama mkwe wake.

115 Akasema, "Rudi kwa watu wako. Mimi ni mzee. Na kama ningewazaa watoto wengine, mbona, . . ." Mnajua torati, jinsi ilivyopaswa kuwa katika siku hizo, ninyi wasomi wa Biblia. Kasema, "Kama ningemzaa mtoto, ingekuwa . . . ungekuwa mzee sana kwake wakati atakapokuwa mtu mzima. Kwa hivyo rudi, nawe unaweza kuolewa tena." Loo, napenda hili.

116 Naomi, sasa, mfano wa kanisa la Kiyahudi. Ruthu, mfano wa Kanisa la Mataifa. Angalieni. Na sasa, huyu hapa anarudi, unaona.

117 Ruthu, akiwa Mmataifa, mwabudu kafiri, alitazama nyuma na kusema, "Nitakwenda pamoja nawe. Mahali unapoishi, nitaishi. Utakapokufia, nitakufa. Mahali utakapozikwa, nitazikwa mimi. Mungu wako na awe Mungu wangu." Hilo ni Kanisa la Mataifa likiukubali wokovu kupitia Yesu Kristo Bwana wetu. Angalia jinsi ilivyo picha nzuri! Na sasa laiti tungelikuwa na wakati.

118 Mlango wa pili, katika Ruthu, unafunua wakati wake wa kurudi, aliporudi wakati tu wa mavuno, msimu wa shayiri. Naye alipoona, alipoitazama nchi ya uenyeji, alilia, "Natamani tu kuingia Palestina!" Unaona, walikuwa wakilia walipoiona ile nchi ya uenyeji.

119 Hao Wayahudi, kwa maelfu, wakimiminika Palestina. Hiyo ndiyo kalenda ya siku hizi, ndugu.

120 Nawaambia, tunaishi mwishoni mwa safari. Sitashangaa hata kidogo kwamba kuna watu wengi wanaoketi hapa, katika umri wa uzeeni, watakaoona wakati ambapo hakutakuwa na jiwe moja lililosalia juu ya lingine, katika Louisville, Kentucky. Hiyo inaweza kuwa katika mwaka mwingine mmoja. Sijui; msiseme nimesema mwaka mmoja. Sijui; hakuna ajuaye. Lakini tuko mwishoni mwa safari. Najua hilo. Hayo mabomu ya haidrojeni na kadhalika yako tayari kulipuka, wakati wowote.

121 Wayahudi wanarudi Yerusalemu. Na nyota yenye ncha sita ya Daudi, ile bendera ya kale sana ulimwenguni, inapepea Yerusalemu, mara ya kwanza kwa muda wa miaka elfu mbili. Ishara ya wakati!

122 Pia, angalieni, kama vile tu Naomi, ambaye alikuwa amepoteza kila kitu alichokuwa nacho, naye alikuwa akirudi tu katika msimu wa shayiri.

123 Nayo Palestina, siku hizi, imeanza kuchanua kama waridi. Baadhi ya vitu vikubwa sana vinapatikana, utajiri wa nchi zote duniani; kemikali, zinazopatikana katika Bahari ya Chumvi, ambazo ni za thamani kubwa. Palestina, nchi kubwa zaidi ya michungwa; ndimu ambazo zitakuwa na uzito wa karibu ratili tano kila moja, zinalimwa humo. Hebu wazia jambo hilo, yote yakitimiza Neno la Kiungu la Mungu! Wakienda nyumbani, Wayahudi, wakirudi katika msimu wa shayiri!

124 Aliinua mikono yake akalia. Nao wakasema, "Huyu hapa Naomi anakuja."

125 Akasema, "Msiniite Naomi, maana Mungu amenitendea mambo machungu," bila kujua alichokuwa akileta. Myahudi hajui ya kwamba kumkataa kwake Yesu kunawapa tu Mataifa nafasi ya kuingia. Loo, ninalipenda tu. Angalieni, basi, alipoinua macho yake, na kulia.

126 Tena angalieni, ndipo ikawabidi kupata. . . Alikuwa amenyang'anywa urithi wake wote, kwa hiyo iliwabidi kuchuma riziki. Ruthu, akiwa msichana mwenye sura nzuri, alienda kwenye shamba la Boazi, kuokota masazo. Hivyo ndivyo wakulima wadogo walivyofanya; walio maskini.

127 Nataka mtambue mfano wa Kanisa. Ni Kanisa maskini. Ruthu, akiwa ni mfano wa Bibi-arusi wa Mataifa sasa, alitoka akaenda nyuma ya wavunaji, kuokota mabua machache yaliyokuwa na ngano; akayapura hivyo, kwenye gunia, apate riziki. Kuokota masazo, miguu mitupu, katika mashamba ya Boazi.

128 Naye Boazi alikuwa bwana wa mavuno, akimwakilisha Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, tazama, Bwana mkuu wa mavuno. Naye akatoka, kuyatazama mashamba yake. Akawaona wakusanya masazo huko nje; akawaona wavunaji. Naye alipomtupia Ruthu macho, akampenda; Kristo, pamoja na Kanisa Lake.

Akasema, "Ni nani msichana huyu anayeokota masazo shambani?" Wakasema, "Ruthu. Akamrudisha tena."

129 Kanisa la Kiyahudi, chini ya uongozi wa Nguzo ya Moto, chini ya uongozi wa Yehova, lilifanya njia, ya Agano la Kale, kwa ajili ya Mkristo wa Roho Mtakatifu wa lile Jipya. Likaja pamoja nao. Loo, tulikuwa na wakati wa kutulia kidogo juu ya hili, angalieni, tukirudi.

130 Kisha akasema, "Mwambie aje aketi chini ya kivuli, apate kula chakula pamoja nasi." Loo, laiti tungelikuwa na wakati wa kutilia hilo mkazo.

131 Angalieni, basi, Boazi anamtazama, akaona alikuwa "mwanamke mwadilifu." Huo bila shaka ulikuwa ni *utakatifu*. Basi akazunguka huku na huku akawaambia wavunaji wote, akasema, "Sasa, nyinyi, wakati msichana huyu anapokuja

nyuma yenu," bila kumjulisha, kasema, "lakini sasa anapokuja nyuma yenu, mara moja moja, angusheni konzi ya ziada ili aweze kuipata." Loo, jamani!

132 Kuzunguka huku na huku, tukiwa na mkutano mdogo *hapa,* na mkutano wa maombi ya kibandani, tukichekwa, tukidhihakiwa na wengine, wavunaji wengine. Tukiokota mabua hapa na pale, na kuyapura. Tukipata baraka kidogo hapa, na kuendesha maili hamsini kwa ajili ya nyingine. Lakini ninashukuru sana kwa ajili ya konzi kubwa mno, mara moja moja, lile Kanisa dogo lililozaliwa mara ya pili linalopata kwenye uamsho wa mtindo wa kale, konzi moja.

133 Alikuwa ameokota hii, nadhani, na kusema, "Bwana asifiwe." Akaipura. Na mnamo usiku alikuwa na gunia zima.

134 Boazi, akimwakilisha Kristo, akaenda mjini, upesi. Hakutaka msichana huyu aondoke. Kasema, "Yeye ni wa nani?"

Kasema, "Naomi."

135 Nalo kanisa la Kiyahudi la Orthodoksi lilizaa Kanisa la Mataifa. Hiyo ni kweli.

Kasema, "Yeye ni nani?"

Kasema, "Yeye ni Naomi." Basi akaenda . . .

136 Ndipo anashuka. Akasema, "Sasa, sina budi kuikomboa mali yake yote." Sasa, sheria ya ukombozi, katika Agano la Kale, kwamba lazima awe ni mkombozi wa jamaa. She—sheria ilihitaji, si mtu yeyote angeweza kuikomboa mali iliyopotea, bali ilibidi iwe ni mtu wa jamaa; halafu mtu fulani ambaye angeweza kukomboa, aliyestahili vya kutosha kukomboa, mwenye uwezo wa kifedha.

137 Ni nzuri jinsi gani! Loo, jamani! Kristo, anastahili, anastahili maradufu! Mfalme wa Mbinguni, akiliona Kanisa dogo, lililojazwa na Roho Mtakatifu, likiangusha konzi ndogo mara kwa mara.

138 Angalieni, jinsi tu ambavyo Mungu angeweza kukomboa, ilimbidi Mungu ashuke na kufanywa jamaa yetu. Mungu alikuwa katika Roho. Mungu alishuka na kufanyika mwili. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Ndipo, ili kumkomboa mwanadamu, ilimbidi awe mwanadamu, jamaa. Je, ungeweza kuwazia Uungu ukishuka, ukifanyika mwili? Upendo!

139 Je, kijana mwanamume atafanya nini kwa bibi-arusi wake ambaye anataka awe mpenzi wake? Yeye ni kipofu. Atafanya chochote. Naam, bwana. Anamtaka. Hakuna kinachoweza kumzuia; atakuwa naye.

140 Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya alipoliona Kanisa. Alilipenda. Hakuna kitu kingemzuia. Alikuwa tayari kuutoa

uhai Wake, naye Mungu akashuka chini katika mwili wa nyama. Anayestahili, Mfalme wa Mbinguni, akawa wa jamaa. Ndipo, Mungu, akiisha kuja katika mwili, katika Yesu Kristo, alifanyika Mkombozi wa jamaa.

141 Mtazame Boazi. Sasa, kabla hajaweza kumpata, ilimbidi kuuliza kama kulikuwako na mtu yeyote, jamaa wa karibu, ambaye angeweza kuichukua, kumchukua. Kwa hiyo kusudi . . . Hapakuwa na mtu yeyote angeweza kufanya hivyo, kwa hiyo basi ilimbidi kutoa ushuhuda wa hadharani mbele ya Israeli, ya kwamba alikuwa amemkomboa Naomi. Naye akamkomboa Naomi, kusudi ampate Ruthu. Loo, jamani!

142 "Alikuja kwa walio Wake, nao walio Wake hawakumpokea." Lakini ilimbidi kumkomboa Naomi, ili ampate Ruthu. Mnaona? Loo, ni picha nzuri jinsi gani! Ati uniambie Neno la Mungu halijavuviwa? Kila sehemu Yake, tukizungumza juu ya kule Kuja!

Naye Ruthu, sasa akingoja.

143 Naye Boazi, mfalme wa mavuno, au bwana wa mavuno, akatoka nje ya malango, akawaita wazee wote wa mji; na kutoa ushuhuda hadharani, nje ya lango. Akasema, "Lizingatieni, ninyi watu wote!" Akavua kiatu chake, akakirusha mbele yao, kama ushuhuda. Akasema, "Mimi, leo hii, nimekomboa urithi wote uliopotea wa Naomi. Na mali zake zote ni zangu, siku hii." Loo, jamani!

144 Jiwekeni tayari, hili hapa. Loo, ninahisi tu kitu kikijongea. Angalieni, Kristo, mbele ya wazee wa Israeli, akiongozwa nje ya malango ya mji, na kutoa ushuhuda. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Ushuhuda wa hadharani, amelikomboa Kanisa kutoka (kitu gani?) mali yake iliyopotea. Katika bustani ya Edeni, hatukuwa na ugonjwa wowote; bustani ya Edeni, hatukuwa na dhambi; bustani ya Edeni, hatukuwa na mauti. "Naye Mungu aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee," akatoa ushuhuda nje ya lango, kwamba alikuwa ameweka njia ya kuepukia kwa wote waliotaka kuja. Ni picha nzuri jinsi gani! Natumaini mnaweza kuiona. Sasa Bwana abarikiwe!

Na kama ninavyoona, labda, muda wangu unaenda.

145 Mungu akifanya njia iliyowekwa, Naye aliifanya katika Yesu Kristo. Yesu alipopanda mlima wa Golgotha, akiwa amejeruhiwa, akitokwa na damu, msalaba ukikokotwa juu ya nyayo za miguu zilizojaa damu alipokuwa akipanda kilima. Akapanda huko; ushuhuda wa hadharani, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Alikufa, akapaa Juu. Mnaamini hilo? Na kurudisha karama za kiroho kwa Kanisa, akifanya njia iliyowekwa. Na furaha hii tuliyo nayo mioyoni mwetu sasa, ni malipo tu ya kwanza, pesa za arabuni, juu ya vile itakavyokuwa tutakapokombolewa kikamilifu. Nao

uponyaji huu wa Kiungu tulio nao sasa ndio arabuni ya ukombozi wetu wa miili yetu. Tumekombolewa. Mungu alitoa Sadaka iliyowekwa.

146 Sina budi kumalizia, enyi marafiki, kwa sababu watu wanainuka na kutoka nje.

147 Nilimwambia mke wangu, hivi majuzi, "Nimehubiri karibu, sijui ni mataifa mangapi mbalimbali, katika kila jiji kote Marekani. Na Louisville, Kentucky ndipo mahali pekee ambapo watu waliwahi kusimama na kutoka nilipokuwa nikihubiri." Hiyo ni kweli, nyumbani, mnaona, mahali pekee ambapo nimewahi kuona.

148 Kama mtu yeyote ameona jambo hilo, ambaye amekuwa katika mikutano mingine pamoja nami, inueni mikono yenu, kote jengoni. Hakika.

149 Huku kote, mahali pengine popote, wala sikuwahi kuwa nalo popote maishani mwangu ila hapa nyumbani kwangu, Louisville, Kentucky. Watu husimama moja kwa moja na kutoka nje, unapoanza kuweka Injili moja kwa moja kwenye mstari wa kukatia. Watafanya hivyo. Wala sijawahi kuwa nalo mahali pengine, popote duniani, nilipopata kuwa; hata Afrika, maeneo mengine yote, Uswidi, Norwe, ambako makumi ya maelfu waliketi. Kwa maoni yangu manyenyekevu, sijawahi hata wakati mmoja kushuhudia mtu mmoja akiondoka, kusimama na kuondoka, huku nikihubiri; ila hapa tu.

150 Mnaona, marafiki, juma hili nimepambana sana kujaribu kuwashawishi baadhi ya watu, kwamba . . .

151 Maneno ya Yesu Kristo, haidhuru ni yapi, hayana budi kuwa kweli. Alisema, "Nabii hakosi kupata heshima isipokuwa miongoni mwa watu wake, nchi yake mwenyewe." Na hiyo ni kweli kabisa. Wao kamwe hawatalipokea. Sijui ni kwa nini. Yesu alisema hivyo, na hilo latosha. Ninao watu kote humu nchini, ambao karibu wangekuwa tayari kufa kwa ajili yangu. Wananipenda. Lakini kwa ujumla, ni Neno la Mungu; naye Mungu hana budi kulitimiza Neno Lake, kusudi awe Mungu. Hiyo ni kweli.

152 Na mtu yeyote ambaye amekuwa kwenye mikutano hapo awali, nje ya hapa, tumekuwa na ishara chache sana na miujiza ambayo imefanywa katika mkutano wowote ambao nimewahi kuona wa—wa kipindi kirefu hivi. Kwa kawaida kuna vipofu, viziwi, mabubu, vilema, na kila kitu, viti vya magurudumu vimelundikana pembeni, na watu wakienda huku na huku, na vitanda vidogo na machela.

153 Na kunao tu, nijuavyo mimi, kumekuwa na watu wawili walioketi hapa. Nilimwona mmoja wao, hapo awali, mvulana huyu hapa, anayeketi hapo. Nilimwona Roho Mtakatifu amesimama juu yake hivi majuzi usiku, akakaribia sana . . . Ningeweza kutangaza uponyaji wake, na wakati tu mimi . . .

kabla sijamaliza kuhubiri; bali nilimwona akimwondokea, akaanza. . . Kitu fulani kilipitia mahali pake pale, kikamzuia. Ndiye mtu pekee ambaye nilimwona angalau akiteseka kwa njia yoyote, nje ya viziwi kadhaa, ama kitu fulani kilichokuja jukwaani, walichoniambia habari zake. Sijui. Lakini haya basi. Ni nyumbani. Ni karibu na watu wako.

154 Sasa, kwa rafiki yangu mwema, Bw. McSpaddin, Bw. McDowell, na wale wanaoketi humu jengoni, usiku wa leo, ambao nimejaribu kuwaambia hili. Nanyi watu huko Jeffersonville, nje ya maskani, je, mnaona ninachozungumzia? Huwezi kulibadilisha Neno la Mungu. Daima litakuwa hivyo, maana Yesu alisema hivyo.

155 Sasa, na kwa watu waliokuwa wakinisihi nirudi maskanini, mnaona ni kwa nini? Ambapo pengine kumekuwa na watu hamsini waliookolewa juma hili, kote huku, katika uamsho; labda si wengi hivyo, labda sio kumi, kwa yote nijuayo. Ambapo, kwa kawaida, katika siku nane, wangeongezeka kwa mamia na mamia na mamia, mahali pengine. Mnaona? Mnaona tofauti yake? Ni nyumbani. Ni miongoni mwa watu wako.

156 Sio kwa sababu hawanipendi, bali kwa sababu Yesu alisema hivyo. "Na wakati alipoenda kwa watu Wake Mwenyewe, jambo pekee aliloweza kufanya lilikuwa ni kuweka mikono juu ya wagonjwa wachache na kuwaponya; asingeweza kutenda kazi kuu." Je, hiyo ni kweli? Hiyo ni kuyanukuu Maandiko. Na hivyo ndivyo haina budi kuwa. Hiyo ni kweli. Sio mimi, hata hivyo. Ni Yeye. Ni Yeye tu. Kama ningekuwa mponyaji. . .

157 Nina ndugu amelazwa hospitalini, usiku wa leo, ambaye Mungu alinionyesha, mwaka mmoja uliopita. Nami nadhani kuna mashahidi mia mbili papa hapa, wa mvulana huyo akiwa mzima na mwenye afya njema. Lakini Mungu alituma ono na kusema, "Anaondoka." Na haijalishi ni nini kitakachotokea, anaondoka.

158 Daktari alisema, si muda mrefu uliopita, "Tunaweza kumwokoa." Lakini hawakuweza, wala hawatamwokoa.

159 Nilimwona Roho Mtakatifu akija, akaonyesha ono, na kuweka alama kwenye kaburi lake, na kusema, "Yeye ndiye anayefuata." Na hivyo ndivyo itakavyokuwa. Ni wangapi walinisikia nikisema hivyo, muda mrefu, mrefu, mrefu sana uliopita? Inueni mikono yenu. Hiyo ni kweli, wakati huyo mvulana alipokuwa mkubwa, mnene, na mwenye afya. Ni lazima tu aondoke. Hakuna lingine. Vipi? Kama ningalikuwa mponyaji, ningemponya. Huyo ni nanii yangu mwenyewe, ndugu yangu mwenyewe.

160 Lakini Mungu akisha kusema, Mungu atalitimiza Neno Lake. Na hiyo ndiyo sababu ninajua kile, BWANA ASEMA HIVI. Nitakufa Nalo, kwa kuwa ni Neno la Mungu Naye atalitunza. Yeye ameandaa Njia, nami nina furaha kuikubali usiku wa leo,

Bwana Yesu Kristo. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Baraka Zake za Milele na zikae juu yenu.

161 Na tena ninasema, Dhabihu ya Mungu iliyoandaliwa, usiku wa leo, njia ya kuepukia, ni kupitia Yesu Kristo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kisha, Yesu Kristo aliandaa kanisa kwa ajili ya wasioamini, ili waweze kuingia na kuona udhihirisho wa ufufuo Wake, na kujua bila shaka yoyote kwamba alifufuka katika wafu. Yesu alifufuka katika wafu, akifanya njia iliyowekwa, kwa yeyote atakaye apate kutazama na kuishi. Lakini kama ukikataa kutazama, unawezaje kufanya chochote ila kufa? Yesu alisema, "Msipoamini kwamba Mimi Ndiye, mtakufa katika dhambi zenu." Hiyo ni kweli.

162 Marafiki, sikuzote nimejaribu kuweka usawa wa barabara. Mnaenda kombo kwenye urasmi, rasmi tu na wa kitamaduni wawezavyo kuwa, watu watanyakua nafasi hiyo. Halafu usipokuwa mwangalifu, utaelekea moja kwa moja upande ule mwingine, na uwe mlokole uwezavyo kuwa. Lakini kuna katikati ya barabara, ambapo Injili ya kweli, imara, ya akili timamu inahubiriwa, na Mungu anaingia mle, akiithibitisha Kweli. "Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, lakini ni wachache watakaoiona." Vema.

163 Kwenu ninyi kundi dogo la watu hapa usiku wa leo, mlioketi hapa, upendo wa Mungu na uwafunike usiku wa leo. Na haswa wagonjwa, wahitaji, ninaomba kwamba kusiwe na mmoja wenu ila atakayerudi nyumbani akiwa mzima. Kama ningeweza kufanya lolote kuhusu hilo, ningelifanya kwa furaha; lakini siwezi kulifanya. Jambo pekee ninaloweza kufanya ni kumwakilisha Yeye kwenu, kwa njia ya karama ya Kiungu.

164 Sasa kama nikisema Kweli, ya kwamba Mungu alitoa Dhabihu; na hiyo Dhabihu, Yehova-Yire, ilikuwa ni Yesu Kristo. Nayo majina yote saba ambatani, majina ya ukombozi yalikaa ndani ya Yesu Kristo. *Yehova-yire,* "dhabihu ya Bwana iliyotolewa." *Yehova-rafa*, "Bwana aponyaye magonjwa yako." Na *Yehova-*. . . "bendera." Na—na mengine yote, majina saba ambatani, yote yalikuwa katika Kristo Yesu. Na hapo ndipo mifano yote na vivuli, vya Agano la Kale, vyote vilikuja na kukutana katika Yesu Kristo. Alilipa gharama kuu, akapaa Juu, kisha akamtuma Roho Mtakatifu kurudi, usiku wa leo, ambaye ndiye njia ya Mungu iliyoandaliwa kwa ajili ya kuepuka kwako.

165 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . tulikuwa na wakati wa kuliingilia.

166 Ninaweza kuwaona mamajusi wakiwapakia ngamia wao, upesi sana. "Kwani unaenda wapi, mpenzi?" anasema mkewe.

167 "Ninaenda kumwona Mfalme mchanga ambaye amezaliwa, mbali huko Palestina."

"Vema, hata hukuchukua dira yako." Akasema, "Sihitaji dira yoyote."

168 "Utapitaje kwenye majangwa, na mabonde, na vilima, bila dira?"

169 Akaelekeza kwenye Nyota, kasema, "Ninapitia njia ya Mungu iliyoandaliwa." Hiyo nyota ikamwongoza moja kwa moja hadi kwa Yesu.

170 Basi sikilizeni, kabla hatujafunga. Mungu anayo njia iliyowekwa hapa usiku wa leo; si kupitia kanisani, si kupitia theolojia. Lakini kwa njia ya Roho Mtakatifu, atakuongoza kwenye njia iliyowekwa na Mungu ya utakaso wako, uponyaji wa mwili wako, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwenye furaha, amani, na kila kitu unachohitaji. Yesu Kristo ndiye dhabihu ya Mungu iliyotolewa.

171 Nami nasema kwamba alifufuka katika wafu, akapaa Juu, akamtuma tena Roho Mtakatifu kama njia ya Mungu iliyowekwa ya kuliongoza Kanisa. Akasema, "Hatanena kwa shauri Lake Mwenyewe, bali atawapasha habari Zangu," Yesu alisema. "Naye atakapokuja, atawakumbusha mambo haya, na kuwapasha bahari za mambo yajayo. Kwa kuwa mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya. Ulimwengu hautaliona, lakini ninyi mtaliona. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari."

172 Usikilizeni, Louisville, Ujumbe wangu wa mwisho kwenu! Dhabihu ya Mungu iliyotolewa ni Yesu Kristo, Yule aliyefufuka hapa akilitia nguvu Kanisa kwa Roho Mtakatifu. Hii ndiyo Nuru. Tembea ndani Yake, upate raha kwa ajili ya nafsi yako, uponyaji wa magonjwa yako.

Na tuombe.

173 Baba wa Mbinguni, Ee Mungu, huku siku . . . Kwenye kilindi cha nafsi yangu, nashangaa, inanishangaza, kuona taifa hili kuu la kupendeza la Marekani, na kuyaona hayo mabomu makubwa huko nje yamewekwa huko ng'ambo ya bahari. Watu waovu, wasio watauwa wanaomkana Mungu, wanamkana Bwana Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, pamoja na uovu wote na fitina, na hila ambazo Shetani anaweza kuzisukuma katika akili zao wapate kuuangamiza ulimwengu huu, wafanye kama vile hasa Wewe ulivyosema ingefanyika, "kuuteketeza kwa joto." Na hata wanasayansi wakuu wa ulimwengu wakisema, "Katika miaka kumi kutakuwa na maangamizi kamili, hakuna atakayesalia, hakuna uhai juu ya nchi; imefagiliwa na bomu la haidrojeni."

174 Ee Mungu, wanaume na wanawake wanaoketi hapa, wasio tayari usiku wa leo. Umekuwa, juma hili, mzuri sana kwetu. Tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, nasi tunakushukuru Wewe kwa ajili ya watakatifu hawa wapendwa huku Louisville. Mungu, jalia watoke kwenye mkutano huu, wakiwa na sauti ya onyo, kwa wote walio karibu.

175 Mpendwa Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamtuma mtu hapa ndani na uamsho wa mtindo wa kale, ambao

utabomoa kuta zilizozunguka Louisville. Ee Mungu, ufanye hivyo. Wapendwa wengi na waletwe kwenye maarifa yaokoayo ya Bwana wetu Yesu Kristo.

176 Nimejitahidi nilivyoweza, Bwana Yesu, yote ninayojua kufanya, nikitoa sauti dhidi ya dhambi kwa bidii nijuavyo, Nawe umekuwa wa kupendeza zaidi kwetu. Umethibitisha kila Neno kwa ishara na maajabu. Tunakushukuru Wewe. Sasa, Baba, kwa ajili ya matokeo, tunayakabidhi yote Kwako. Mapenzi Yako yatimizwe.

177 Mbariki Ndugu Cauble, Bwana, ndugu yetu. Wabariki wafanyakazi wake wote, na wahudumu wengine wote. Tunamwazia maskini Ndugu Durban, hapa chini, na hawa ndugu wengine karibu na hapa, ambao ni ndugu wazuri; wakijaribu wawezavyo kuishambulia dhambi na uovu, wiski na ulevi, na kufanya mabaya, na kukusanyika, ama kila kitu kote mjini. Wanajaribu kutoa sauti ya onyo. Mungu, wabariki watu hao na uwatie mafuta kwa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Jalia wawe watumishi wazuri, wenye mafanikio makubwa ya kuwaita watu watoke gizani, waingie kwenye nuru ya ajabu.

178 Na sasa, Bwana, katika hii ibada ya kumalizia, usiku wa leo, hivi hutakuja? Njoo mara nyingine tena, Roho Mtakatifu mkuu, Nguvu za Kiungu, na utufunike kwa baraka Zako. Pia jalia Malaika wa Mungu asimame hapa jukwaani, kama shahidi wa ufufuo wa Dhabihu iliyotolewa na Mungu, Bwana Yesu Kristo. Na jalia afanye ishara kubwa na maajabu, katika kulithibitisha Neno. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake, Mwanao mpendwa, Yesu Kristo. Amina.

179 Bwana na akubariki, rafiki Mkristo. Sasa nataka kuwaombea wagonjwa. Ninataka kuwaulizeni sasa, mapema tu. Je, kuna mtu mmoja aliyeko humu jengoni, ambaye hajaokolewa, bado, hata angalau kuongoka, wakimwomba Kristo awasamehe dhambi zao? Ninakuomba kwa njia wazi, yenye kuparuza. Nami ninaamini ya kwamba utakuwa mwanamume ama mwanamke vya kutosha, ama mvulana au msichana, kufanya jambo hilo. Ikiwa hujawahi kumkubali Yesu kama Mwokozi wako binafsi, na unataka kufanya hivyo sasa, naomba usimame kwa miguu yako kama Mwaminio, na kusema: "Mimi sasa, tangu saa hii, nitakuwa mwaminio katika Yesu Kristo." Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama.

180 Unakiri imani yako katika Yesu Kristo, unapofanya hivi. Yapata watu watano, kama wangalikufa dakika tano zilizopita, wangeingia katika Umilele mweusi. Kama wakifa sasa, wamefunikwa na Damu.

181 Mwingine mmoja, ni wapi? Huku nyuma kabisa, Mungu akubariki. Naam, ndugu yangu. Mungu akubariki, ndugu. Huyo, Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni kweli. Ninii

tu ya kale inayoparuza . . . Mungu akubariki, ndugu, kumkubali Yesu. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Juu kwenye roshani, mahali fulani? Mungu akubariki, dada.

182 Hiyo ni nzuri sana. Loo, jamani! Laiti tungelikuwa na nafasi hapa kwa ajili ya benchi ya waombolezaji wa mtindo wa kale na wito wa madhabahuni. Hiyo ndiyo tunayohitaji sasa hivi.

183 Ni wangapi humu ndani wanaosema, "Ndugu Branham, nimekuwa mwenye dhambi, lakini sasa ninaungama, nikikubali moyoni mwangu, Yesu Kristo, dhabihu iliyotolewa na Mungu"? Takriban dazeni mbili wamesimama. Je, utasimama na kusema . . . Mungu akubariki. Mungu akubariki, kijana. Hilo ni sawa. Mungu akubariki. Mtu mwingine asimame, na kusema, "Sasa ninamkubali Yesu Kristo sasa hivi, kama Mwokozi wangu. Ninafanya maungamo haya waziwazi, mbele ya watu na mbele za Mungu, kwamba sasa ninakubali tiba ya Mungu kwa ajili ya dhambi yangu, Yesu Kristo." Je, kunaweza kuwako na mmoja zaidi, hapa, popote? Mungu akubariki, kijana. Huo ni ushujaa. Mungu akubariki. Hilo ni sawa.

184 Mtu mwingine angesimama, aseme, "Sasa ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu binafsi, ninachukua dhabihu iliyotolewa na Mungu kwa ajili ya dhambi yangu"? Mungu akubariki, baba; mzee, mwenye mvi, akitetemeka, anainuka kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi.

185 Sasa, Mungu anaujua moyo wako; anakuangalia moja kwa moja. Mungu akubariki, kijana. Nilikuona pale, ukiwa umevaa sweta nyekundu, ukiinuka juu. Vema, mtu mwingine, inuka na useme, "Nakubali." Mungu akubariki, na wewe, huyo mama na huyo mvulana mdogo hapo juu. Mungu akubariki. Mungu na . . .

186 Jina lako linaingizwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo unaposimama hadharani mbele ya kusanyiko hili. "Yeye atakayenikiri Mimi mbele ya wanadamu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu. Kama ukinionea haya Mimi hapa mbele ya wanadamu, nitakuonea haya kwenye Siku ile."

187 Je, umekuwa mwenye dhambi, na unataka kusamehewa? Mtu mwingine yeyote ambaye bado hajasimama, na anataka kusimama, kukubali tu dhabihu ya Mungu iliyotolewa kwa ajili ya dhambi yako, je, waweza kusimama? Baadhi . . . Mungu akubariki. Mungu akubariki. Huyo ni mvulana askari. Mungu akubariki hapa, pia. Bwana awe nawe, ndugu yangu.

188 Mtu mwingine anaweza? Vema. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, dada. Hilo ni sawa. Mtu mwingine anayetaka Uzima wa Milele, kwa kumkubali Yesu Kristo? Mungu akubariki. Naam. Mungu awabariki, ninyi watatu, juu kwenye roshani.

Je, hiyo si ni ajabu? Thelathini, au zaidi, sasa. Vema.

189 Mungu akubariki. Hiyo ndiyo njia, kumkubali Yesu, Dhabihu ya Mungu iliyotolewa. Yeye ni Yehova-Yire. Vema. Bwana akubariki huko kwenye roshani, dada yangu, akupe Uzima wa Milele.

190 Sasa unapata kibali kwa Mungu. Hakuna Mkristo humu ndani, ambaye anajua chochote kuhusu Mungu, asiyejua kwamba dakika tano zilizopita, mazingira yamebadilika, kabisa, katika jengo hili. Hiyo ni kweli. Mnaona? Katika wakati huo tu wenye giza kabisa, ndipo Yesu anakuja.

191 Mtu mwingine aseme, "Sasa ninamkubali Yesu Kristo. Mimi . . ." Mungu akubariki, mama. "Ninamkubali, nataka jina langu liandikwe kwenye Kitabu Chake. Ninamkubali sasa hivi kama mtawala wangu mkuu wa maisha yangu." Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki.

192 Mtu mwingine, aliyerudi nyuma, angesimama na kusema, "Wakati mmoja nilikuwa Mkristo, Ndugu Branham, lakini nimesafiri mbali, mbali na Mungu. Usiku wa leo, naja Nyumbani"? Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, ndugu. Loo, Mungu anakuona. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Mungu akubariki, ndugu; ninakuona kwenye roshani. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu aliyeinua mikono yake juu. Mtu mwingine? Mungu akubariki, mama. Hiyo ni ajabu. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni ajabu. Hiyo ni . . . Endeleeni tu kuja. Na Mungu akubariki, dada; nakuona ukisimama. Mungu akubariki, bwana, hapo juu jukwaani, umeinua mkono wako. Mungu akubariki.

193 Huko nyuma, huko nyuma kabisa, hivi mtu anaweza kusema, "Ndugu Branham, sasa nimerudi nyuma; naja Nyumbani. Ninakubali tiba yangu, Yesu Kristo, dhabihu iliyotolewa kwa ajili ya kurudi nyuma kwangu. Naja Nyumbani, usiku wa leo. Ninalitatua hapa, sasa na hata milele. Nami najua kwamba wakati . . ."? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> Fungua wazi mikono Yako ya upendo,
> Bwana, naja Nyumbani.
>
> Naja Nyumbani, naja Nyumbani,
> Kamwe sitatangatanga tena;
> Fungua wazi mkono Wako wa upendo,
> Bwana, naja Nyumbani.

194 Sijui kama tunaweza kuuvumisha.

195 Wakati wakiuvumisha, kunaye mtu hapa, aliyebaki, angesema, "Bwana, unaniona ninaposimama. Naja Nyumbani sasa. Nimechoka na kutangatanga huku, kuhangaika. Ninaikubali njia Yako ya kutokea, Yesu Kristo kama Mwokozi wangu. Sasa naja, Bwana, jinsi nilivyo. Naja; nainua mkono wangu. Nitasimama na kukuacha Wewe uone, pamoja na

wasikilizaji hawa, ya kwamba sasa ninaamini, nami naja Nyumbani"? Mungu akubariki, dada.

Naja Nyumbani, naja Nyumbani, kamwe. . .

196 Yeyote anayejisikia moyoni mwao kwamba wanataka kumkubali Yeye, simama tu kwa miguu yako.

Fungua wazi mkono Wako wa upendo,
Bwana, naja Nyumbani.

Endelea tu, ukipenda, dada.

197 Nitawaulizeni jambo fulani sasa. Kila mtu aliyesimama, ninakutaka usimame kwa miguu yako ninapokuombea. Kila mtu aliyesimama, simama tena, kwa dakika chache tu. Simama tu, kila mahali kote jengoni. Kila mtu aliyesimama, simama tena, kila mahali, roshani na kila mahali, ili tuweze kuomba. Ndivyo hivyo. Ndivyo hivyo. Kila mmoja wenu aliyesimama, aliyesimama muda mfupi uliopita. Na endapo kuna wengine zaidi wanaotaka kusimama pamoja nao, wakimkubali Kristo, naomba usimame sasa. Mungu akubariki.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

198 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, hawa sasa wanakuja kama watoto Wako. Tayari wamekuja. Mara Roho Mtakatifu aliponena na nafsi zao, walisimama na kukukubali Wewe, Nawe ukawapa Uzima wa milele. Mungu, wabariki. Tembea pamoja nao maishani, Baba. Baadhi yao wamekuwa watumishi Wako, nyakati zilizopita, lakini wameanguka; na, usiku wa leo, Roho Mtakatifu, kwa kuhubiriwa kwa Neno, ameshuka na kuwatia mafuta. Nao sasa wanasimama, wakikukubali Wewe, na kukushukuru kwa ajili ya Uzima wao wa Milele walio nao sasa katika Yesu Kristo. Asante, Baba. Maisha yao na yawe ya furaha na matamu. Ugonjwa usiukaribie mlango wao. Na waishi maisha marefu, yenye furaha; kisha waje kwa amani, katika Ufalme wa Mungu, mwishoni mwa ulimwengu. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

199 Mungu awabariki. Nao watu wakasema: [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Amina." Mungu ambariki kila mmoja. Ikiwa umeketi karibu na mtu aliyesimama; wape mkono, Mkristo, na uwaambie jinsi unavyowafurahia.

200 Hatuna nafasi hapa, kuwaita kuzunguka madhabahu. Kamwe hatuna na—nafasi hapa kufanya hivyo. Bwana awabariki; watu wengi, wengi sana.

201 Sasa mnajua, kulingana na Neno la Mungu, imekuwaje Mbinguni wakati huu? Malaika wanashangilia. Bendera nyeusi za Shetani zimeshindwa; zimeshushwa na zikafukuzwa. Nao Malaika na bendera zao nyeupe za ushindi zinapepea Mbinguni usiku wa leo, nazo kengele za Utukufu zinalia, zinaimba tu nyimbo tamu, wakati mwenye dhambi mmoja akimjia Kristo. Bwana ahimidiwe na asifiwe milele! Loo, jamani!

202 Ninaamini tu tutakuwa na ibada halisi ya uponyaji sasa. Naam? Ati nini? Kadi za maombi? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

203 Mimi, kama mtumishi Wake, ninaiweka kila roho, humu jengoni, chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sababu ya kusema hivyo, hiyo inaliweka Jina la Yesu Kristo juu ya kusanyiko lote. Kama Shetani angefanya ukaidi, mngeona kile kingetokea. Pengine wangewabeba wawapeleke nje ya mlango, kutoka katika ulimwengu huu, mnaona.

204 Sasa, kwa hiyo lazima uwe mtiifu. Usiamke na kutembea-tembea. Kaa kimya. Magonjwa haya hutoka kwa mtu mmoja yakamwingia mwingine. Mwajua, wasomi wa Biblia, ya kwamba hiyo ni kweli. Mnaona? Sio kucheza kanisa sasa. Wala siwajibikii wakosoaji au wasioamini. Nisikilizeni! Ninazungumza katika Jina Lake.

205 Sasa, Malaika wa Bwana, yu karibu, ninatumaini ya kwamba Mungu atadhihirisha ufufuo wa Mwanawe.

206 Sasa jongea karibu. Nadhani, dada, mimi na wewe tukisimama hapa pamoja, ya kwamba hatufahamiani. Sikujui wewe. Sijawahi kukuona. Lakini Mungu anatujua sote wawili. Wewe ni mtu tu ambaye alileltwa kutoka kwenye kusanyiko. Baadhi yao walikupa kadi ya maombi, iliyokuwa na namba juu yake. Ulipata tu namba yako, nayo ikaitwa, nawe huyu hapa.

207 Wala haikubidi kuwa na hiyo kadi ya maombi. Yeyote anayeketi kwenye kusanyiko, anza tu kuomba; uone kama Roho Mtakatifu si yeye yule tu usiku wa leo, aliye kanisani, aliyekuwa juu ya Yesu Kristo. Uone kama siye. Endapo siye, endapo siye, basi nimeiwakilisha Injili vibaya kwenu, ndipo ninakuwa shahidi wa uongo wa ufufuo. Kama Mungu akithibitisha kwamba ni Kweli, basi nimesema Kweli, na Mungu amesema ni Kweli.

208 Sasa, huyu mama hapa, mgeni, sijawahi kumwona maishani mwangu. Hajawahi kuniona, nadhani. Tumekutana tu hapa, hivyo tu. Simjui. Mungu anamjua.

209 Sasa, wakati Bwana wetu Yesu alipokuwa hapa, Yeye alizungumza na mwanamke fulani wakati mmoja, hakuwa amewahi kumwona maishani Mwake. Alikuwa akiteka maji kisimani. Naye akasema, “Nipe maji ninywe.” Naye akazungumza na mwanamke huyo muda mrefu vya kutosha kuishika roho yake, kisha akamwambia shida yake ilikuwa wapi.

Naye akasema, “Vema, naona ya kwamba Wewe u nabii.”

210 Sasa, Yesu alisema, “Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya, hata mwisho wa ulimwengu.”

211 Mtu mmoja alikuja kwenye mstari Wake wa maombi, wakati mmoja; alikuwa mtu mwadilifu. Akasema, "Wewe ni Mkristo, mtu mwema, mtu mwenye heshima."

212 Akasema, "Ulinijua lini, Rabi?" Au, "Kasisi, Mwalimu," vyovyote unavyolitafsiri.

213 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Kwa maneno mengine, "Uliomba kabla ya kuja kwenye mkutano, nami nikakuona ukifanya jambo hilo."

214 Akasema, "Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli."

215 Sasa kama Yesu amefufuka katika wafu, basi atafanya vivyo hivyo.

216 Sasa, wasikilizaji, sasa Yeye yuko hapa, Malaika wa Bwana. Mnafahamu hilo sasa, kwamba jambo fulani lilifanyika wakati huo. Je, hiyo si ni kweli? Hiyo ni kweli. Yuko hapa?

217 Sasa, kuwaponya, singeweza. Maisha yako usingeweza kuyaficha, kwa kuwa huko mbele ya ndugu yako; ni katika Uwepo Wake. Hiyo si ni kweli? Nawe unamwamini kwa moyo wako wote, ya kwamba Mungu ametutuma hapa kujaribu kukusaidia. Mbali na kuwa mgonjwa, wewe mwenyewe, una mpendwa ambaye ni mgonjwa. Huyo ni mumeo. Ana henia, sivyo? Naam. Nyote wawili mmeponywa. Mnaweza kwenda nyumbani sasa. Mungu awe nawe na akubariki. Mungu akubariki, dada.

Imani rahisi ilimgusa na kumponya huyu mwanamke.

218 Njoo. U hali gani, dada? Nadhani hatufahamiani. Hatujuani. Sasa, mimi ni ndugu yako tu. Ni kwa ajili ya mtoto wako mchanga, ndilo limekuleta hapa. Kivuli cheusi kinaning'inia juu ya huyu mtoto. Ugonjwa wake hautibiki, kulingana na madaktari. Je, unaamini anaweza kunifunulia tatizo la huyu mtoto mchanga? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Kwa moyo wako wote, unaamini? ["Ndiyo, bwana."] Kumekuwa na aina fulani ya tukio la hospitalini. Mtoto huyo amefanyiwa upasuaji. Na ni kitu kwenye matumbo. Na kuna namna fulani ya mfupa au chochote kile ambacho hakiko sawa. Naye mtoto amevimba ini sasa. Je, hiyo si ni kweli? ["Ndiyo, bwana."] Hiyo ni kweli, sivyo? ["Ndiyo, bwana."]

219 Sasa, huyo si mimi niliyesema hivyo. Hiyo ilikuwa ni kujitolea kikamilifu kwa Yesu Kristo. Nao Uwepo Wake upo hapa. Sasa jambo pekee niwezalo kufanya ni kumwomba Mungu kwa ajili ya mtoto wako. Unakubali uponyaji wa huyo mtoto? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.]

220 Kristo, Mwana wa Mungu, mrehemu mtoto huyu anayekufa. Na apate afya usiku uu huu. Jalia, Bwana Yesu, kwamba baraka Zako zije juu yake naye atakuwa mzima, kwa kuwa ninaomba haya katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

221 Mungu akubariki, mama. Hebu nisikie kuhusu huyu mtoto, li—lililotukia. Utapata tofauti ndani yake, katika saa ishirini na nne zijazo. Sasa kumbuka niliyokuambia. Yeye ajuaye kilichokuwako, anajua kitakachokuwa. Vema.

222 Njoo, mama. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba Bwana Yesu Kristo yuko hapa kuponya na kuwapa afya? Je, unaniamini kama mtumishi Wake? [Dada huyo anasema, "Naamini."—Mh.] Unafahamu ya kwamba uko katika Uwepo wa kitu Fulani mbali na mwanadamu, na hicho ni Roho Wake.

223 Kusanyiko linaweza lisielewe hili. Lakini angalieni sura ya mgonjwa anapojongea hapa. Si kwa sababu ni mimi; sina uhusiano wowote nalo. Mimi ni sauti tu. Lakini mwanamke huyu hapa, ama yeyote wa hao wengine, anaelewa na anajua ya kwamba kuna kitu cha kimbinguni hapa. Na unaweza kukiona kama mwujiza. Mwujiza ni nini? Kitu ambacho hakieleweki.

224 Sasa, huyu mwanamke, hanifahamu, nami simfahamu huyu mwanamke; hatufahamiani; mara ya kwanza maishani kukutana, labda. Lakini Mungu ametulisha sisi sote wawili tangu tulipozaliwa.

225 Mama, unaamini ya kwamba, Bwana Yesu yeye yule aliyezungumza na yule mwanamke kisimani, ambaye nimemwakilisha hapa usiku wa leo, ambaye mia tatu... au watu mia moja na watatu walimkubali kama Mwokozi? Je, unaamini sasa kwamba Yeye anaujua moyo wako, na anajua kila kitu ambacho umefanya? Ikiwa atanifunulia kile unachohitaji sasa, utakubali? [Dada huyo anasema, "Nitakubali."—Mh.] Fadhaa. Hiyo ni kweli? ["Hiyo ni kweli."] Unaniamini sasa? ["Hakika ninakuamini."] Sasa hili hapa jambo lingine. Unamjali mpendwa, ambaye ni mvulana. Na mvulana huyo ana shida ya moyo. Naye ni mshiriki wa kanisa hapa Louisville, kanisa la Kibaptisti. Nenda, Bwana Yesu akubariki na akupe shauku ya moyo wako. Amina.

[Ndugu mmoja jukwaani anasema, "Semeni, 'Bwana asifiwe.'" Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe."—Mh.]

226 Kuwa na uchaji tu; kubali, amini.

227 Sasa ninamwona mama, mwanamke mweusi, ameketi, akiomba. Ana shida ya figo. Hunayo sasa, mama. Imani yako imekuponya. Simama. Mungu akubariki. Amini tu, kwa moyo wako wote, nawe utaupata.

Roho Mtakatifu, dini ya Agano Jipya! Amina.

228 Unaamini kwamba shinikizo hilo la damu litakuacha, bwana; unayeketi hapo, ukiniangalia? Naam. Vema, unaweza kuupata. Mungu akubariki.

Mwamini tu Yeye.

229 Amini, dada, unayeketi hapo ukiangalia huku, ukiomba, pia. Una kasoro kooni mwako, sivyo? Unayeketi moja kwa moja nyuma ya huyo msichana mdogo hapo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, maskini mama unayeketi hapa? Umeketi hapo ukiniombea niseme jambo fulani kwako. Najua ni tatizo la koo lako. Huhitaji kadi ya maombi. Unahitaji tu kile ulicho nacho, imani. Je, unakubali uponyaji wako sasa? Mungu akubariki. Nenda nyumbani ukapone sasa. Amina.

230 Kuwa na imani! Amini kwa moyo wako wote; Yesu Kristo atalitimiza. Loo, ninampenda, nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

Njoo, bwana.

231 Mwamini Mungu. Amini kwa moyo wako wote. Mungu atalitimiza.

232 U hali gani, bwana. Je, ulikuwa mmoja wa waliosimama, dakika chache zilizopita? Naona bado kuna Nuru imekuzunguka. Ulimkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi. Unasumbuliwa na hali ya fadhaa. Sivyo? Umekuwa na tabia mbaya, kuvuta sigara. Mungu hataki ufanye hivyo. Hiyo inaidhuru mishipa yako, ikikufanya ufanye hivyo. Je, hiyo si ni kweli? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Ukitaka kufaulu; achana na sigara, achana na kila kitu. Yesu Kristo amekwisha kuugusa mwili wako, nawe utakuwa mzima na kumtumikia. Unaamini sasa?

233 Ili uweze kujua hili. Wewe hutoki kwenye mji huu. Unatoka nje ya mji, sivyo? [Ndugu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Umetoka Indiana. Ulivuka mto. Unatoka katika mji uitwao Greensburg, ama kitu kama hicho, Indiana. Je, hiyo ni kweli? Sasa uko sawa. Naam. Sasa unaweza kwenda nyumbani na kuwa mzima. Mungu akubariki.

234 Kusanyiko liwe na uchaji, iweni katika maombi, iweni mkimtarajia Mungu kuwabariki na kuwaponya. Amina. Mwaminini Mungu!

235 Wewe unayeketi hapo, mama, umeinua kidole chako juu namna *hii,* ukiugua ninii. . .Je, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya msukumo huo mdogo wa damu ulio nao? Je, unaamini? Naam. Unaamini Yeye yuko? Simama kwa miguu yako basi na ukubali. Utakuacha, nawe unaweza kwenda nyumbani na kuwa mzima.

Unasema, "Ni nini kilichosababisha hilo?"

236 Yesu Kristo yeye yule aliyemgeukia yule mwanamke mwenye kutokwa na damu, akasema, "Imani yako imekuokoa." Kasema anajua mambo yote, Naye anayafunua atakavyo. Vema.

Mlete mgonjwa wako. Aminini.

237 U hali gani, bwana? Je, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? [Ndugu huyo anasema, "Naam, ninaamini, bwana."—Mh.]

Unaamini uko katika Uwepo Wake, si wa ndugu yako. Lakini unajua kuwa kitu fulani kinaendelea? ["Naam, bwana."]

238 Mtu fulani alisema nilikuwa nasoma mawazo yako wakati uo huo. Hilo si kweli. Yesu Kristo "alitambua mawazo yao." Hiyo ni kweli? Watu hawawazii dhambi zao na mambo waliyofanya. Ni Roho Mtakatifu.

239 Vema, angalia huku, bwana, na uamini. Sisi hatufahamiani? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Hatufahamiani. Labda hatujawahi kuonana maishani mwetu mwote. ["Ni katika mkutano huu tu."] Mkutano huu tu. ["Hiyo ni kweli, bwana."] Basi kama kuna jambo lolote kukuhusu wewe ama chochote kile, ugonjwa wako ama chochote kile, Mungu pekee ndiye awezaye kujua. Kwangu mimi, sijui.

240 Lakini ninakuona ukipelekwa hospitalini. Umetoka tu hospitalini hivi punde. Kuna tatizo kwenye damu, chembedamu kuvunjika, au kitu fulani. Na umekuwa . . . Ninakuona kitandani, na kuna kitu fulani kinachoning'inia karibu nawe, ni kitu kinachotonesha . . . Ni damu. Ninaona mara moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba ambazo umeongezwa damu hivi punde. Hiyo ni kweli? [Ndugu huyo anasema, "Hiyo ni kweli. Huyo ni Bwana."—Mh.] Ni kweli.

241 Una mke ambaye ni mgonjwa. Ana yabisi kavu, na ugonjwa wa ini. Je, hiyo ni kweli? [Ndugu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Nawe hutoki kwenye jiji hili. Umetoka upande wa juu wa mto, kutoka Cincinnati, Ohio. Jina lako ni Berghaus. R.P. ndizo herufu zako za kwanza. Rudi nyumbani ukapone, Yesu Kristo amekuponya.

242 Mwaminini Mungu! Ati kumwambia jina lake? Je, Yesu Kristo hakumwambia Petro, "Wewe ni Petro"?

243 Sasa iweni na kicho, enyi marafiki. Maono yanakufanya dhaifu sana. Mumekuwa mikutanoni, juma hili, nanyi mnajua ninachozungumzia. Mwaminini tu Mungu! Aminini! Na kulikuwa na kitu . . . Hebu kidogo.

244 Ninaona mwanamke mbele yangu. Hapana, ni—ni mwanamke huyu anayeketi papa hapa mwishoni. Wewe ni . . . Sio wewe; ni mtu mwenye sura tofauti. Ni mpendwa aliye hospitalini, nao wana kansa. Na ni mwanamke, naye yuko katika hali ya kufa. Naye ni shemeji yako. Je, hiyo ni kweli? Ikiwa ndivyo, simama kwa miguu yako sasa na ukubali kuponywa kwa shemeji yako hospitalini. Bwana Yesu Kristo ajuaye yote juu yake!

245 [Dada mmoja anashangilia—Mh.] Vema, dada, wewe unayepiga makofi, ukishangilia. Mikono yako ilikuwa na tatizo fulani, sivyo? Vema, imeponywa sasa, nawe unaweza kwenda nyumbani.

246 Nawe unayeketi karibu naye hapo, ulikuwa na mawe ya nyongo. Sivyo, mama, unayeketi hapo? Simama kwa miguu yako. Unaweza kwenda nyumbani, pia, na kuponywa. Yanakuacha, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

247 Amini tu! "Yote yanawezekana kwao waaminio." Mwamini Mungu!

248 Mlete huyo mama. Unaamini, mama, unapokuja? Unamkubali Yesu kama Mwokozi, na kunikubali kama nabii Wake?

249 Basi ikiwa hiyo ni kweli na nimeshuhudia juu ya ufufuo wa Yesu Kristo; Yeye aliyesimama na kuzungumza na yule mwanamke kisimani, alijua shida yake hasa. Akasema, "Nenda kamwite mumeo." Mwanamke akasema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia kila kitu nilichowahi kufanya." Kamwe hakumwambia yote aliyowahi kufanya. Lakini Yeye alijua, kwa kuwa Baba angemfunulia, yote aliyowahi kufanya. Je, Yeye ni Bwana Yesu yeye yule aliyefufuka?

250 Umekuwa na ajali. Hapana, una kitu kinachoonekana kama ni. . . Umekuwa. . . Unamtafuta Roho Mtakatifu, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Nawe una ninii. . . Nilikuwa nimeona kitu fulani, una—una shinikizo kuu la damu, pia, sivyo?

251 Hebu kidogo, ono lilitokea mbele yangu. Loo, ni yule mwanamke anayeketi pale, akiomba. Ni wewe uliyekuwa na. . . Umeumiza mguu wako, sivyo? Ajali, ukaumiza mguu wako. Je, hiyo ni kweli? [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Na una tatizo la figo. Je, hiyo ni kweli? ["Ndiyo."] Njoni huku, pamoja na huyo mama, nyote wawili mtapona. Yesu Kristo. . .

252 Haleluya! Loo, Bwana Yesu Kristo mtukufu, asiye na kifani, aliyeokoa nafsi yako muda mfupi tu uliopita, anathibitisha Uwepo Wake. Amina. Chunguzeni kwenye kanda zenu zilizorekodiwa mwone kama anachosema si kweli. Loo, mwamininі Mungu! Amini! "Mambo yote yanawezekana kwao waaminio."

Vema, Billy, huyu ndiye mgonjwa wako? Mlete.

253 Unaamini, kwa moyo wako wote? Una mpendwa aliye na tatizo, pia, sivyo? Hawako hapa katika jiji hili, pia. Wana namna fulani ya mazoezi ya viungo. Ni ngoma ya Mt. Vitasi, kitu kama hicho. Hiyo ni kweli? Na wanaishi katika mji ambao kuna mto. Ni mji mkubwa, na kuna mto unaopitia kando yake. Na kuna mengi sana ya mada-. . . Ni St. Louis. Hiyo ni kweli? Ni kweli.

254 Nawe una jamaa mwingine, ambaye ni dada au kitu fulani, naye anatoka katika nchi iliyo na vilima ndani yake, miti isiyokauka. Ni Arkansas. Naye ana ugonjwa wa moyo. Nenda, shauku zako umepewa na Yesu Kristo Mwana wa Mungu.

255 Hebu tuseme, "Bwana Yesu Kristo asifiwe, Yule aliyefufuka, Yule aliyetoka Kalvari!"

256 Iweni na kicho, msisogee. Dakika moja tu, nasi tutafunga katika dakika chache. Msisogee humu hivyo, inafanya, inanikatiza. Nina ninii...hapa usiku wa leo, nikitazama. Iweni na kicho.

257 Hebu huyo mama aje. Je, unaamini ungeweza kupona, kwa imani, na uvimbe huo ungekuacha pasipo kufanyiwa upasuaji? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Unalikubali sasa? Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe kwako kama vile imani yako imesema. Amina.

258 Bwana, uliyeketi hapo, umevalia tai nyekundu; unaugua he—henia. Unaamini ya kwamba Bwana Yesu anakuponya? Unakubali? Umetoka nje ya mji, pia. Ninakuona ukitoka upande wa juu wa mto, pia, Cincinnati. Hiyo si ni kweli? Vema. Huku nyote wawili mkifanya kazi, nyote simameni kwa miguu yenu sasa hivi na mkaponywe katika Jina la Yesu Kristo. Mungu awabariki. Umewaacha. Nendeni nyumbani; mkapate afya.

259 Njoo, mama, ukiwa na imani. Unaamini kwamba tatizo hilo la kike limekuacha? Je, unamkubali Yesu kama mponyaji wako sasa? Hilo lilikuwa jipu, lilikuwa na mtiririsho, na lingegeuka hivi karibuni kuwa kansa. Lakini imani yako imekuokoa. Sasa nenda, mpe Mungu sifa kwa ajili yake, nawe utapata lolote uombalo.

260 Njoo, bwana, ukiamini kwa moyo wako wote. Ikiwa Mungu atafunua tatizo lako ni lipi, utakubali uponyaji wako? Ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli? Unaamini anakuponya sasa? Basi, Yeye anakuponya. Imani yako inakufanya mzima. Nenda, kwa amani ya Mungu.

261 Njoo, mama. Unaamini Mungu atamponya mtoto huyo ninapokuja kupitia jukwaani? Ana ugonjwa wa figo. Nenda sasa, Yesu Kristo anamponya mvulana huyo mdogo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Ulikuwa na wasiwasi; huo umekuacha, pia. Mungu awe pamoja nawe.

262 Mnamwamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mwaminini Mungu!

263 Unataka kuondokana na ugonjwa huo wa mkamba? Unaamini Mungu anakuponya huo? Kama unaamini kwa moyo wako wote, simama kwa miguu yako, mama. Kubali uponyaji wako. Mungu akubariki. Unaweza kwenda nyumbani sasa na kuponywa. Vema. Unaamini kwa moyo wako wote? Je, utakubali uponyaji wako ikiwa Yesu Kristo, akizungumza, atafichua shida yako? Hatufahamiani, lakini, Yeye anajua shida yako. Una shida ya wanawake, mwanamke, tumbo na ovari. Sasa, nenda, Mungu amekuponya. Imani yako inakuokoa, mama, katika Jina la Yesu Kristo.

264 Hebu tuseme, “Bwana asifiwe!” [Kusanyiko linasema, “Bwana asifiwe!”] Kila mmoja wenu anaweza kuponywa wakati huu, kama mtaamini.

265 Sasa, mama, simama ulipo, angalia huku. Kusanyiko hili lote, asilimia kubwa yao, linakabiliwa na fadhaa hiyo. Wakati mwingine unafikiri utarukwa na akili, sivyo? Unashikwa na fadhaa sana. Hivi majuzi uliangusha kitu fulani; kilikuwa ni sahani ama chochote kile, ulikuwa ukienda nacho. Lakini sasa Yesu Kristo amekuponya huo, nawe unajua hilo. Sasa nenda zako, ukishangilia.

266 Sasa, katika Jina la Yesu Mwana wa Mungu, ninampa changamoto kila mwaminio humu ndani kuamini ya kwamba hii ni Kweli. Je, mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, basi, kama hii ni Kweli ya Mungu iliyothibitishwa, nisikieni. Wekeaneni mikono, ninapowaombea. Nami nataka kila mtu humu ndani sasa ukubali uponyaji wako.

267 Mwenyezi Mungu, uwarehemu wagonjwa na wanaoteseka. Nikisimama hapa, na chumba hiki chote kinaonekana kuwa Nguzo moja kubwa ya Nuru sasa. Nikijua kuwa mtu fulani amesimama karibu huku mikono yao imenizunguka, imewekwa juu ya leso; zibariki, Bwana, kwa uponyaji wa wagonjwa. Watu hawa wote wahitaji hapa, huku wamewekeana mikono. Jalia zile Nguvu, njia iliyowekwa na Mungu, Mwana wa Mungu, katika Nguvu Zake kuu na ukuu, zipitie humu jengoni kama upepo mkali ukienda kasi, na—na kuhukumu kila ugonjwa, zitoe kila pepo mchafu.

268 Sasa ninamhukumu Shetani, ninadai ushindi dhidi yake sasa hivi. Basi, Shetani, toka ndani ya watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo.

269 Na hebu kila mmoja humu ndani, anayeamini ya kwamba Yesu huwaponya, wasimame kwa miguu yao na kumpa Mungu sifa, katika Jina la Yesu Kristo.

270 Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, sasa wanakubali uponyaji wao.

54-0404E Mungu Anayo Njia Iliyowekwa
Memorial Auditorium
Louisville, Kentucky Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org